

HUMBOLDT FORUM

# KUONYESHA. KUTOKUWEPO

## VITU KUTOKA TANZANIA NA NYARAKA ZA KIKOLONI

KITABU CHA MAZOEZI


S
W
O
N
Jakarta
Manila
Bangkok
Dhaka
Mumbai
Delhi
Tokio
Peking


Kapstadt
Johannesburg
Pretoria
Antananarivo
Luanda
Daressalam
TANSANIA
Dodoma
Kinshasa
Libreville
Douala
Abidjan
Lagos
Addis Abeba
Dakar
Khartum
Timbuktu
Riad
Kairo
Bagdad
Rabat
Teheran
Algier
Istanbul
Madrid
Rom
Paris
London
Berlin
Moskau

Kitabu hiki cha mazoezi kinajumuisha maonesho ya hivi karibuni ya "Kuonyesha.Kutokuwepo – Vitu kutoka Tanzania na Nyaraka za Kikoloni", ambayo yalioneshwa kwenye maonesho ya Humboldt Forum kuanzia Septemba mwaka 2022 hadi Juni mwaka 2024. Maonesho yaliandaliwa na Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss kwa kushirikiana na Ethnologisches Museum na Zentralarchiv der Staatlichen Museen zu Berlin – Preußischer Kulturbesitz, na yalifadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Kamishina wa Utamaduni na Vyombo vya Habari yaani kwa misingi ya kuleta upatanisho iliyopendekezwa na kusainiwa na Bunge la Ujerumani.

Ushauri wa kikosoaji uliongozwa na Josephine Apraku na Vicensia Shule.

Jalada: Indeksi ya Historia Kuu, "Liste der Objekte einer ostafrikanischen Würdenträgerin aus Urugu" (Orodha ya vitu alivyomiliki Mwanamke mashuhuri wa Afrika Mashariki kutoka Urugu)

Ukurasa ya 2 na 3: Ramani ya Dunia, 2022

| | |
|---|---|
| UTANGULIZI | 6 |
| "HAKUNA RIDHAA – HAKUNA KITU?" WARSHA YA MAONESHO | 8 |
| HISTORIA | 14 |
| KUVUMILIA USUMBUFU | 22 |
| NYARAKA | 34 |
| "NI NGUMU" ? | 56 |
| KUINGILIA KATI | 68 |
| HITIMISHO | 78 |
| KUTAMBUA MCHANGO | 80 |
| HISTORIA YA MRADI | 81 |
| ORODHA YA PICHA | 83 |

**Mada: Washauri Wakosoaji kwa ajili ya "Kutathmini kwa Kina Mkusanyiko wa Vitu Vilivyochukuliwa Afrika Mashariki" (MK)**

Mpendwa,

Tunakuandikia ili kukujulisha kuhusu mradi wa "Kutathmini kwa kina Mkusanyiko wa Vitu Vilivyochukuliwa Afrika Mashariki" (mada ya kufanyia kazi) ambao kwa sasa umepangwa na Ethnologisches Museum (EM), SMB-SPK, na Stiftung Humboldt Forum (SHF). Mradi huu ambao utahusisha warsha shirikishi, umepangwa kufanyika katika mrengo wa Mashariki wa Humboldt Forum kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2022 na kuendelea. Tunataka kuanzisha kikundi cha washauri wakosoaji ili watusaidie kwenye maonesho na tungependa kuwaomba wachukue jukumu hili. Kabla hatujakuuliza kama ungependa kushiriki katika nafasi hiyo ya mshauri mkosoaji tungependa kukushirikisha mradi huu kwa njia ya mkutano mfupi wa masafa. Je, tunaweza kupata miadi yako kwa ajili ya kufanya kikao hiki kwa lengo hilo?

Muundo wa warsha utakuwa wa kukarahisha, unaouliza maswali kwa ajili ya kukabiliana na aprasia ya kikoloni. Tungependa kuifanya kazi yetu kwa kuongozwa na msingi wa "Hakuna Ridhaa – Hakuna Kitu?". 'Mali zinazomilikiwa kitamaduni' hazitaoneshwa endapo vizalia wa Kitanzania wa wazalishaji, watumiaji, au wamiliki wa 'vitu', (mamlaka) wadau, na jamii husika hawajatoa idhini zao. Nyaraka za kikoloni pamoja na simulizi zenye misingi ya kibaguzi kuhusu "ugawaji" wa mkusanyiko wa vitu vilivyochukuliwa kutoka Afrika Mashariki inabidi viwekwe hadharani.

Tungependa kushirikiana nawe kwa ajili ya warsha na mjadala unaolenga kuchunguza ni kwa vipi Washauri Wakosoaji wanaweza kuchangia kwenye miradi ya maonesho. Tunatazama namna unavyoweza kutusaidia kwa kushiriki katika kuunda wazo, uzalishaji wa vipindi katika vyombo vya habari, usanifu wa maonesho, programu ya maonyesho, ukosoaji muhimu, muundo wa elimu, na warsha. Pia unaweza kuchagua jukumu ambalo halikufanyi uonekane waziwazi kwamba umeshiriki katika programu hii. Ushiriki wako kupitia mijadala na ushauri, warsha, muundo wa tukio, kuingilia kati, n.k. yatakuwa ni majukumu yatakayolipwa.

Tunatamani kutengeneza jukwaa lenye manufaa na lenye kuthamini utu katika Humboldt Forum huku tukizuia – na/au kuvuta hisia – zozote za umamluki.[2]

Tunatumaini kwamba utachangia maoni yako na mtazamo wako tunduizi na tungependa kukushirikisha mradi huu kupitia mkutano wa mtandaoni kwa njia ya simu.

Natanguliza shukrani za dhati,


Paola Ivanov (Ethnologisches Museum Berlin, SMB), Kristin Weber-Sinn (Zentralarchiv, SMB), Jocelyne Stahl, na Maike Schimanowski (Stiftung Humboldt Forum)

[1] Matumizi ya neno "mali zinazomilikiwa kitamaduni" hayaakisi vifaa ambavyo thamani yake inazidi hadhi ya vitu vya kawaida. Hata hivyo, neno hili linamaasisha tofauti bandia kati ya kazi za sanaa na "vitu"/ "ethnografia" ambavyo siyo vya kisanaa. Izingatiwe kwamba matumizi ya istilahi hii ni kwa mpito tu kwa kuwa inatumika alama ya mnukuo mmoja kwenye neno 'kitu' au linaweza kuwakilishwa na kishazi kama "mali zinazomilikiwa kitamaduni".

# UTANGULIZI

Katika msimu wa kuchipuka majani mwaka 2021, sisi – timu ya wahifadhi ambao ni wanawake wanne weupe[3] ambao ni wasomi na waajiriwa wa taasisi za makumbusho – wataalamu wabobevu, wanachama wa dayaspora na wanaharakati, tuliungana na kufanya kazi hii. Lengo letu lilikuwa kuwakaribisha ili wachukue jukumu la kuwa *washauri Wakosoaji* ambao wangeweza kutupatia ukosoaji na kusaidia katika mchakato wa kuandaa maonesho ya "Kuonyesha.Kutokuwepo – Vitu kutoka Tanzania na nyaraka za Kikoloni".

Japokuwa watu wengi waliijibu vizuri baruapepe yetu, wengi walikataa kushiriki katika mradi wa Humboldt Forum. Hivyo tulishukuru sana watu wawili tuliowasiliana nao na kuwaomba wawe washauri wa mradi katika warsha ya "Kuonyesha.Kutokuwepo" na pia baadaye walihusika katika uingiliaji kati wa masuala ya sanaa ikiwemo mvuto wa kisinema pamoja na vifaa vya kuhifadhia sauti, video fupi ya filamu ya makala kutokana na mtazamo wa *washauri wakosoaji*, na kitabu cha mazoezi ambacho hivi sasa umekishika mikononi mwako.



Picha 1



[2] "Umamluki" ni istilahi inayotumika kufafanua mchakato wa taasisi kuhusisha wawakilishi wa makundi ya watu wachache kwa ajili ya lengo la kuhadaa kwamba taasisi hizi zinazingatia uanuai na ujumuishwaji. Kwa kufanya hivyo, wanashindwa kushughulikia matatizo sugu kwenye taasisi zao kama vile ubaguzi. Hawa watu wanaalikwa kama "mamluki", na mara kadhaa ushawishi wao hauna tija na pia hawahusishwi katika ngazi za maamuzi. Kwa hiyo taswira chanya ya taasisi kwa nje haiakisi ukweli wa mfumo uliopo ndani ya taasisi hiyo.

[3] Weupe katika muktadha huu siyo istilahi ya kibinafsi. Tungependa ieleweke kwamba weupe ni mtazamo wa kijamii ambao hauhusiani na maumbile ya kiasili. Weupe unamaanisha nafasi ya kimamlaka na ya hadhi ya juu katika mfumo wa kibaguzi (tazama futiwayo namba 4 kuhusiana na istilahi "Weusi").

# HAKUNA IDHINI – HAKUNA KITU? WARSHA YA MAONESHO

Tunawezaje kupata huduma za utunzaji wa makumbusho ya ethnolojia hivi sasa na kutuwezesha kufuatilia na kufanya utafiti – na hatimaye kuonesha kwenye maonesho – 'vitu' vilivyoporwa wakati wa vurugu chini ya ukoloni wa Mjerumani kwenye eneo la kiutawala ambalo kwa sasa ni Tanzania? Hili ni swali ambalo sisi timu ya wasimamizi (wanataaluma weupe na waajiriwa wa Staatliche Museen zu Berlin and Stiftung Humboldt Forum) tulijiuliza sisi wenyewe wakati wa msimu wa joto mwaka 2020. Katika kipindi hicho ilikuwa ni wazi kabisa kwamba kuna haja ya kufanya maonesho yanayolenga *Historia za Tanzania* (mada bado inafanyiwa kazi) tukishirikiana na Makumbusho ya Taifa la Tanzania, ambayo yaliahirishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Korona. Je sisi tungewezaje kupata dhamira hii bila kushirikiana na wataalamu kutoka Tanzania na wanadayaspora?

Tukaamua kuanzisha warsha kwa ajili ya mijadala na mabadiliko. Katika maonesho ya "Kuonyesha. Kutokuwepo", ambayo yalianzia Septemba mwaka 2022 hadi Juni 2024 huko Berlin's Humboldt Forum, tulilenga kwenye 'vitu' vya kihistoria na kitamaduni vilivyoibwa, kuporwa, kunyang'anywa, kununuliwa, na kupewa kama zawadi na/au kufanyiwa biashara katika muktadha ambao haukuzingatia mahusiano ya kiusawa kati ya mtawala na mtawaliwa. Zaidi ya vitu 10,200 vinavyoonekana kwenye daftari la kumbukumbu vilichukuliwa kutoka Tanzania ambavyo kwa sasa viko chini ya mamlaka ya Makumbusho ya Ethnolojia Berlin, na zaidi ya asilimia 80 ya vitu hivi vilichukuliwa wakati wa enzi za utawala wa kikoloni wa Mjerumani na Mwingereza.



## HAKUNA IDHINI

Pamoja na "mafaili ya upatikanaji wa taarifa", picha, kanzidata, katalogi, na vyanzo vingine vya taarifa, hizi namba zinamaanisha nyaraka ambazo hazijakamilika na wala siyo thabiti. Katika nyaraka hizi za kikoloni tuliona mifano ya itikadi za kikoloni na vurugu: zilizowakilishwa kwa ujinga, kuondoa vitu, lugha za kibaguzi, pamoja na kategoria za Kiulaya. Hiki ndicho kitu tunachotaka kionekane waziwazi. Na wakati huohuo, tunataka kuzingatia upinzani wa watu dhidi ya vurugu za utawala wa kikoloni katika koloni lililojulikana kama "Afrika Mashariki ya Ujerumani". Tunavutiwa kwa namna fulani kwa watu na jamii ambako 'vitu' hivi viliibwa.

## HAKUNA KITU

Hatujaonesha 'vitu' halisi na nyeti ambavyo bado hatujapa ridhaa ya vizalia wa wazalishaji, watumiaji, walezi, au wamiliki. "Kutokuwepo" katika maonesho haya imewakilishwa kwa rangi ya pinki. Kwa namna hii tunataka kuonesha kwamba nyaraka si kamili bali ni vipande na hazina wigo mpana kulingana na mtazamo wetu na kuhusiana na mada hii. Kwa namna hii tulitaka kutengeneza jukwaa kwa ajili ya majadiliano.




Picha 2

Ukitathmini kiyakinifu ukatili wa kikoloni na muundo wa mamlaka na ukiangazia matokeo ya itikadi ya ubaguzi wa rangi ambayo bado tumebakia nayo sisi hadi leo hii, ndicho kichocheo kikubwa cha dira ya Humboldt Forum. Kwenye jengo ambalo siyo asilia bali limejengwa kwa upya na linajumuisha sehemu ya fakadi ambayo ilitumiwa kama Kasri la Kifalme la Berlin, tutafanya uwasilishaji kiyakinifu wa hivi 'vitu' na historia zake, jambo linaloweza kuibua ubaguzi wa rangi na muundo wa kimamlaka nyuma ya upatikanaji wa hivyo vitu, ni kazi ngumu lakini ni muhimu. Kama eneo hili, kasri la kihistoria linawakilisha utawala wa Kifalme wa Prussia na ulihusishwa kwa karibu na nguvu za kijeshi, ukoloni, na ukandamizaji wa harakati za kidemokrasia.

Kama timu ya wahifadhi binafsi ambao ni weupe ambao wamekulia Ulaya na hawajaambukizwa hisia za ubaguzi wa rangi, tunachukua jukumu hili la kuhatarisha usalama wetu kwa kufanya maonesho haya yanayorudia muundo wa ndani wa mfumo wa kibaguzi kwa misingi ya rangi. Matokeo yake, tulihitaji msaada zaidi kwa kuungwa mkono ili kuanzisha jukwaa hili, na waliotunga mkono ni wataalamu wawili kutoka Dar es Salaam na Ujerumani.

## NI KWA JINSI GANI MAONESHO YAMEPANGWA KUFANYIKA NA 'MAKUSANYO YA VITU' YA MAKUMBUSHO AMBAYO NDIYO MHIMILI WA MAONESHO LAKINI HAYAONESHWI?

Na Szandra Tebbe (Studio Ra)

Kulikuwa na maswali mengi pale mwanzoni tulipoanza mchakato wa kuratibisha jambo hili. Ili kuboresha jambo hili kwa kutumia lugha ya staha na ya kibunifu, sisi kama waratibu wa tukio hili tulitaka kuelewa muktadha wa maonesho yajayo.


## NI KWA VIPI WAGENI WANAOKUJA KUTEMBELEA HUMBOLDT FORUM WANAELEWA KUHUSU UKOLONI WA WAJERUMANI? JE WAGENI WANAIJUAJE TANZANIA? JE, VYUMBA VINGINE VYA MAONESHO YA MAKUMBUSHO YA ETHNOLOJIA VINAONEKANAJE KWENYE UPANDE WA 'AFRIKA'?

Kwa kuzingatia jukumu la mchakato wa maandalizi ya maonesho ilimaanisha pia kugundua kutokuwepo kwa mtu binafsi: je, sisi kama waandaaji tunawezaje kufahamu kuhusu ukoloni wa Wajerumani huko Tanzania?  Tulipojadiliana jambo hili mwanzoni mwa ushirikiano wetu mwaka 2020, tuligundua kwamba sisi tunajua vitu vichache sana. Tukadhania kwamba jambo hili pia linawatokea wageni wanaokwenda kuitembelea Humboldt Forum.



Ushirikishwaji ulikuwa ni mbinu muhimu kwetu sisi waandaji wa maonesho. Kwa upande wa usanifu, hii inamaanisha kwamba maarifa hayapaswi kupokelewa kibwete bali kwa ushiriki hai. Wageni wahusishwe katika mchakato wa maandalizi ya warsha, katika mwendelezo wa mjadala wa kutokuwepo. Kwa kusaidiwa na wenzetu wenye mtazamo mpya, ilitarajiwa kwamba itawawezesha kujua kutokuwepo kwao binafsi na hivyo wataweza kuchukua nafasi zao.

Mfano mmojawapo ni uchunguzi kuhusu mada ya picha za kikoloni: katika vibanda vya maonesho, safu kadhaa za paneli huwekwa na kuangazwa na kitambaa na kuangazwa na picha kwa mbele. Wageni waliingia kwenye kibanda kwa kutembea kupitia ule mwangaza na hivyo nao wakawa sehemu ya taswira inayojiakisi. Maelezo ya kina kuhusu motifu yanatolewa nyuma ya paneli. Nia ilikuwa ni kuhimiza kujiuliza na kutafakari kupitia uzoefu wa milango ya fahamu.




Picha 3


## TUNAWEZAJE KUONDOA UKOLONI KWA MACHO YETU WENYEWE?

Dhana ya "Hakuna Idhini - Hakuna kitu?" inatupatia changamoto ya namna tulivyozoea kuviangalia vitu. Tathmini ya asili ya 'vitu' imesaidia kutoa mtazamo yakinifu katika uwasilishaji wa 'kazi bora' za makumbusho. Hii inaunga mkono simulizi za Kimagharibi kuhusu mtazamo wao kuhusu 'vitu'.

Usanifu haushughulikii tu tabia mahususi za 'vitu' bali ukweli kwamba 'vitu' havikutengenezwa kwa ajili ya kuoneshwa kwenye makumbusho au kwenye vibanda vya maonesho. Inaonekana kuwa huu usanifu ulifanywa ili kustaajabia 'vitu' pasipo kupata taarifa za awali juu ya vitu hivyo.

Kwa kuzingatia haya akilini tuliamua kubadilisha uwasilishaji wa kawaida wa makumbusho kwenye vibanda vya maonesho ili kuonesha utata wa 'vitu'. Alama za 'vitu' ambazo kwa namna fulani zimekusudiwa kutoa muhtasari mfupi kadri inavyowezekana na usanifu wake umewekwa kwa namna isiyo dhahiri, zinapaswa kuonekana kama hatua 'zinazosukuma' kioo cha kibanda cha maonesho.

Wanatakiwa wawepo na kwa wingi ili kupitia idadi yao, watuwezeshe kupata mitazamo tofauti ya 'kitu' na kusisitiza kwamba 'kitu' cha 'mkusanyaji' kinabeba hadithi tata ndani yake. Jina la 'mkusanyaji' au taarifa za vifaa na ukubwa wake ni kiwakilishi tu cha ngazi mojawapo au mtazamo.





Picha 4

13

## JE, RANGI INA DHIMA GANI KATIKA MAWASILIANO YA DHANA YA WAHIFADHI?

Dhana ya wahifadhi na maswali waliyoyaibua wameyawekea msimbo wa rangi au kupigiwa mstari kwenye matini. Lengo kuu la hizi alama lilikuwa kufanya mabadiliko ya ukoloni yawe dhahiri na hivyo kuvutia usikivu wa wageni katika uhusiano huo: Nafasi ya "Hakuna Idhini – Hakuna kitu?" iliwekewa alama kwa rangi ya kijani na ikawekwa sehemu ya mbele ya maonesho kwenye kibanda ambacho kiko wazi (hakina kitu).

Vifungu na muktadha unaoelezea kuhusu kutokuwepo kwa vitu vingi ambavyo vilipatikana kwa kutumia vurugu, ujinga na kukosekana kwa taarifa katika matini hii kumepigiwa mstari wa pinki. Kwa kuongezea, baadhi ya mbinu za kibunifu zilitumika ili kupata uzoefu wa kusimulia kutokuwepo: kupitia maswali huru, vielelezo, vyumba vikubwa vilivyopakwa rangi ya pinki, tafakari na uzalishaji kiubunifu wa 'vitu'.




Picha 5

"Safari ya siku mbili na kuendelea, kuna soko la mwisho kabisa la bara la Azania, ambalo linaitwa Rhapta; ambalo jina lake linatokana na boti zilizoshonwa (rhaptôn ploiariôn) zilizotajwa tayari; ambamo ndani yake kuna pembe nyingi sana, na ganda la kobe."

*The Periplus Of the Erythraean Sea, Travel and Trade in the Indian Ocean by A Merchant of the First Century,* iliyotafsiriwa kutoka kwenye Kigiriki na kufafanuliwa na Wilfred H. Schoff, New York: Longmans, Green, and Company, 1912



Watu waliokuwa wanaishi katika pwani ya Afrika Mashariki wamekuwa wakitumia misafara ya utumwa kupitia Bahari ya Hindi tangu karne ya kwanza AD. Vioo, shanga, sarafu na vyombo ya udongo vimeshuhudia kuwepo kwa karne nyingi za kibiashara kati ya bahari ya Madeterranian, India,

Asia ya Kusini-Mashariki, China, na ghuba ya Arabia. Biashara ndicho kilichounganisha wakazi wa pwani na wale wa maeneo ya ndani kama vile Falme za Zimbabwe na Mapungubwe (Afrika Kusini).

Katika eneo la pwani na kisiwani mbali na pwani, kulianzishwa masoko na miji. Rhapta, ambayo inatajwa kwenye nukuu, lilikuwa ni eneo lililokaliwa na watu ambalo kwa sasa tunaweza kusema ni Tanzania au Kenya na walitembelewa na wafanyabiashara kutoka Arabia ya Kusini. Miongoni mwa bidhaa zilizochukuliwa kutoka Rhapta ni pembe za ndovu. Ibn Battūta, msafiri wa karne ya kumi na nne kutokea Afrika Kaskazini, alielezea mji wa kibiashara wa Kilwa (tazama picha 4) uliopo Kusini mwa Tanzania kama mojawapo ya kivutio cha kifahari na hakuna mwingineo kama huo.

Kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na tano na kuendelea wafanyabiashara wa Kireno na wasafiri wa majini walijaribu kudhibiti biashara kwa nguvu. Walijenga ngome na kushambulia kwa mabomu na kuteka miji ya pwani. Miaka mia mbili baadaye, mtawala wa Omani aliwafukuza Wareno na akajitangazia utawala wa eneo la pwani – isipokuwa mamlaka ya Msumbiji ya leo. Mwaka 1840

walihamisha makao yao makuu na kuyapeleka Zanzibar. Katika maeneo ya ndani athari yao ilikuwa hafifu.

Hivi leo leo Tanzania inakaliwa na makabila yapatayo 120. Mbali na lugha rasmi za Kiswahili na Kiingereza, kuna lugha nyingi zinazozungumzwa nchini Tanzania. Jamii ya Waswahili ("watu wa pwani") inajumuisha watu na mawazo kutoka kwa jamii za Waafrika Mashariki na wale wa Bahari ya Hindi. Uanuai wa kiutamaduni unajiakisi kupitia mavazi, majengo, vyakula, lugha, na dini ya Kiislamu kwa kutaja kwa uchache. Katika maeneo ya bara nchini Tanzania kulikuwa na mifumo mingi ya kiutawala katika jamii ikiwemo falme katika jamii wa Kaskazini-Magharibi hadi kwenye jami zilizokataa viongozi wa kisiasa, hairakia na mifumo ya kudhibiti ya serikali kuu.

Historia ya jamii za Afrika Mashariki zina sura nyingi kuliko mipaka halisi iliyopo sasa ya Tanzania ya leo. Vyanzo vingi vya Kiulaya-Kimarekani vya wakati wa ukoloni na vya muktadha wa mara baada ya ukoloni vilijikita katika mikoa ya pwani. Hata hivyo, historia simulizi na tafiti za kiakiolojia, zinafichua picha tata ya historia na mifumo ya jamii za Afrika Mashariki.





Picha 6

"Mpaka hivi karibuni historia ya Afrika Mashariki kabla ya mwaka 1800 imewasilishwa kama historia ya majimbo ya miji ya pwani na uhusiano wao na biashara ya Bahari ya Hindi. Nchini Tanzania umakini mkubwa umekuwepo Kilwa na Zanzibar. Hii haijawa hivyo kwa sababu maeneo ya ndani hayakuwa yakikaliwa na watu, lakini kwa sababu wanahistoria walikuwa wakiangalia tu rekodi za maandishi na eneo la pwani lilitokea kuwa na rekodi chache aidha katika mfumo wa historia au rekodi za wasafiri waliotembelea pwani katika kipindi hiki."

Isaria N. Kimambo. The Interior before 1800. kwa: Kimambo na Temu (wahariri), A History of Tanzania. Nairobi: East African Publishing House, 1969



Picha 7

„Ubepari unahusisha kukosekana kwa usawa na ubaguzi wa rangi unachochea jambo hilo […] Ubepari wote unahusisha ubaguzi tangu mwanzo wake […] na utaendelea kutumia misingi ya kibaguzi na utawala wa kimamlaka wa kibaguzi bila kujali lolote.“

Ruth Wilson Gilmore, Profesa wa Mafunzo ya Dunia & Mazingira na Mafunzo ya Kimarekani, City University of New York, kutoka Geographies of Racial Capitalism with Ruth Wilson Gilmore, An Antipode Foundation film directed by Kenton Card, https://antipodeonline.org/geographiesof-racial-capitalism/



Jamii za Afrika Mashariki zilizokuwa maeneo ya bara zilijihusisha na uchumi wa kibepari duniani kupitia biashara ya masafa marefu ya karne ya kumi na tisa. Misafara ya kibiashara ilianzia pwani hadi Ujiji katika Ziwa Tanganyika, hadi Ziwa Nyasa, na kupitia (historia) Ufalme wa Buganda hadi Congo. Pembe za ndovu zilikuwa ndiyo biashara kubwa kwani zilibebwa na watu wengi, na baadhi yao walikuwa ni watu waliochukuliwa utumwani. Utumwa ulifikia kilele chake katika karne ya kumi na tisa. Watu waliochukuliwa utumwani huko Zanzibar walilazimishwa kulima karafuu kwa ajili ya soko la dunia.

Nguo za pamba zilianza kuingizwa katika Afrika Mashariki. Kuanzia miaka ya 1880, bunduki zikawa muhimu sana, na kila mwaka silaha za moto zilizoingizwa zilikuwa 100,000.

Ndani ya kipindi kifupi Afrika Mashariki ikawa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, na kiutamaduni. Vikundi vikubwa vya kisiasa vikaundwa ambapo utajiri na nguvu za kijeshi vikawa ndiyo msingi wa umaarufu wa kisiasa. Wanyamwezi ni mfano mmojawapo wa jamii hizo. Misingi ya asili na ya kizamani ya kiutawala kama vile uongozi wa kurithishwa na mamlaka za kutambika, zikaanza kutiliwa shaka kuhusu uhalali wake na hilo likapata umaarufu wake.

Katika kipindi hiki, wasafiri wa Ulaya, watafiti, na wamisionari walifuata njia za misafara ya kibiashara na kujizoeza njia za usafirishaji za vijijini na mikoani na hivyo wakazitumia njia hizo kwa ajili ya malengo yao wenyewe. Hawa ndiyo waliowezesha mazingira ya kutawaliwa na wakoloni.

Mchakato wa ukoloni uliofanywa na Ulaya kupitia utumwa, kupokonya ardhi, na unyonyaji wa rasilimali ulianza miaka mia tano iliyopita. Haya maendeleo yalichochewa na mkutano wa Berlin (1884 / 85) ambapo wanadiplomasia wa Ulaya na wanasiasa waliweka misingi ya kuigawanya Afrika. Miongo iliyofuatia mipaka iliyoonesha mgawanyo wa maeneo iliwekwa bayana kwa kuanzisha kwa nguvu sheria za kikoloni, na dola za kiutawala zikaanzishwa.

Miongoni mwa maeneo yaliyodaiwa ni ya Himaya ya Mjerumani ni eneo la sasa la Tanzania bara. Tangu mwanzoni, watu wa Afrika Mashariki walipinga matumizi ya nguvu yaliyotumiwa na majeshi ya Kijerumani kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1880 na kuendelea. Kampeni za kijeshi kama "msafara wa kuvamia", udhalimu, kazi za kulazimishwa, na kulipishwa kodi ya mkoloni vilikuwa ni vichocheo (na alama mahususi) ya utawala wao uliolenga unyonyaji kiuchumi kwa kuwanyonya watu na rasilimali zao. Wajerumani walikabiliana na upinzani huo wa watu wa Afrika Mashariki kwa ukatili mkubwa.

Watu wa Afrika Mashariki kupitia maeneo ya Kusini mwa Tanzania ya sasa ambao walishiriki katika Vita vya Maji Maji (1905–1907), ambao wanakadiriwa kuwa 300,000 ama waliuawa au walikufa kutokana na uharibifu mkubwa uliokuwa umefanywa kwenye makazi yao.

Katika Vita vya Kwanza vya Dunia, jeshi la Kijerumani – lililokuwa na askari wake Waafrika, lilipigana na majeshi ya Mwingereza na ardhi ya Afrika Mashariki – ikageuka kuwa uwanja wa vita. Maelfu ya watu wa Afrika Mashariki walipoteza uhai. Baada ya Mjerumani kushindwa katika vita hivyo, mamlaka ya Tanzania bara ya sasa, yalikabidhiwa chini ya utawala wa Mwingereza kupitia Umoja wa Mataifa na kwa kipindi hicho ilijulikana kama Tanganyika.





Picha 8

"Mimi sina mahusiano na wewe na sikumbuki kama ulinipa pesa au robo pesa au sindano au uzi. Ninatafuta sababu kwa nini ninapaswa kuwa mtiifu kwako na sielewi hata kidogo. Kama ni swala la urafiki tu, mimi sina kinyongo, leo na siku zote, lakini siwezi kuwa chini yako [...]".

Machemba bin Mshame Masaninga kwa Hermann von Wissmann, Gavana wa Afrika Mashariki ya Ujerumani; hati isiyokuwa na tarehe [pengine 1890 au 1891] na iliyotafsiriwa kwa Kijerumani, Bundesarchiv R 1001/473

"Ninakuambia hivi tunataka Uhuru. Na hatuwezi kupata Uhuru ikiwa hutaki kujiunga na chama. Tumewazaa wanaume hawa wote. Wanawake ni nguvu katika dunia hii."

Bibi Titi Mohamed akiwahutubia wanawake wa kikundi cha Bombakusema, Mnamo mwaka 1955 (?), Dar es Salaam (Susan Geiger. TANU Women. Portsmouth N. H.: Heinemann, 1997)

"Watu walipigana kwa sababu hawakuamini katika haki ya mzungu ya kuwatawala na kuwaongoza watu weusi. Walianzisha uasi mkubwa si kwa kuogopa harakati za kigaidi au kiapo cha ushirikina, lakini kwa kuitikia mwito wa asili, mwito wa roho uliovuma katika mioyo ya watu wote, na nyakati zote, kwa waliosoma na ambao hawakusoma ili kupinga kutawaliwa na wageni."

Julius K. Nyerere. „Statement to the U.N. Fourth Committee, 1956", kwa: Nyerere. Freedom and Unity. Dar es Salaam: Oxford University Press, 1966

Harakati za kupigania uhuru zikaanza kujitokeza Tanganyika kwenye miaka ya 1950: Chama cha Tanganyika African National Union (TANU) kikaundwa. Rais wake alikuwa ni Julius Kambarage Nyerere. Wanasiasa wengineo kama vile Bibi Titi Mohammed waliwahamasisha watu kuhusu uhuru ili kuachana na ajira ya Mwingereza. Kaulimbiu yao ilikuwa Uhuru na Umoja. Tanganyika ikajipatia uhuru wake mwaka 1961 na kisha ikaungana na Zanzibar na kuwa Tanzania mwaka 1964.

Lengo lililokusudiwa lilikuwa ni kujenga umoja na hivyo Ujamaa ukaanzishwa, ambayo ni istilahi ya Ujamaa wa Kiafrika. Miongoni mwa mambo yaliyofanyika ilikuwa ni kukomesha mifumo yote ya unyonyaji na kutaifisha mali ili zimilikiwe na umma kwa njia ya kidemokrasia na kimshikamano. Mara nyingine malengo hayo yalitekelezwa kwa nguvu kinyume na matakwa ya watu. Wanasiasa wanaamini kwamba misingi ya Ujamaa wa Kiafrika ilitokana na historia ya Waafrika kabla ya kutawaliwa na wakoloni.

Mfumo wa Chama kimoja cha siasa ukaanzishwa nchini Tanzania na mfumo huo ulivunjwa mwaka 1992. Ili kutimiza matakwa ya Benki ya Dunia (World Bank) na Shirika la Fedha Duniani (International Monetary Fund) serikali ya Tanzania ikaamua kuachana na misingi yake ya usawa kijamii, kiuchumi na kisiasa mwaka 1980 ili kutimiza matakwa ya uchumi wa kiliberali mamboleo.

NOTSI ZANGU

"Hakuna Idhini – Hakuna Kitu?"
Kauli mbiu ya maonesho hayo, Berlin, Septemba 15, 2022
Sehemu hii ya onesho ni tupu. Kwa upande wa vitu vingi kutoka Tanzania vinavyoshikiliwa na Jumba la Makumbusho ya Ethnolojia Berlin hatuna uhakika kama kuna kibali cha kuviwasilisha katika maonyesho. Lakini nani yupo kwenye nafasi ya kutoa ruhusa au kibali? Swali hili linatumika kama hatua ya kumalizika kwa maonesho ya warsha hii. Kwa sababu hii, tuliamua kutokuonesha hadharani vitu vya asili mpaka tukiwa na kibali cha kufanya hivyo.



Picha 9





Picha 10

Grafu hii inaonyesha vitu vingi (mali) vya kitamaduni kutoka katika nchi ambayo kwa sasa ni Tanzania ambavyo viliporwa katika kipindi cha upanuzi wa koloni la Mjerumani (kuanzia miaka ya 1880) na utawala wake kuanzia mwaka (1885–1919) na kisha vikapelekwa huko Königliches Museum für Völkerkunde – ambako kuna makumbusho ya kienthrolojia ya kifalme – huko Berlin (kwa namba ya kumbukumbu c. 7,000). Katika miaka ya 1930, wakati wa utawala wa kikoloni wa Waingereza, uongozi imara wa Kinazi na mhakiki wa kikoloni Ludwig Kohl-Larsen aliporwa 'vitu' zaidi ya 1,300 ambavyo alivipeleka kwenye makumbusho huko. Sasa kuna zaidi ya namba za kumbukumbu c. 10,232 kwenye kanzidata ya Ethnologisches Museum ambazo zinarejelea 'vitu' vilivyochukuliwa enzi hizo kutoka eneo la sasa la Tanzania.

Moyo wa Giza – Moyo wa Ulaya

Moyo wa Giza unapatikana katika sehemu sawa na Moyo wa Ulaya: uliozikwa kwenye kina kirefu, chini zaidi ya miamba. Inaweza kupatikana karibu na kuta, mwishoni mwa korido za vilima, nyuma ya milango mizito. Sehemu ambayo ni ngumu kupumua. Sehemu ya mazishi ambapo viumbe hai, na historia yao imezikwa. Katika sehemu ya maonesho, nyuma ya vioo, vilivyopangwa katika kategoria ambazo ni agano la wajinga, simulizi ambayo watu ambao siyo weupe wali-shikiliwa kama mateka.

Josephine Apraku, 2022



Picha 11 – 16



Uingiliaji huu wa kisanii unatokana na wazo la washauri wa kukosoa na timu ya waangalizi.

Imetolewa na:
Josephine Apraku: Mkurugenzi wa sanaa, Mkurugenzi
David Buchholz: Mkurugenzi wa upigaji picha, Mkurugenzi msaidizi, Mhariri, Mtayarishaji
Vincent Engel: Meneja
Simone Nowicki: Msanii wa folei
© Apraku, Buchholz, Nowicki, 2022
Utayarishaji wa video na tellsomemore production

# PICHA YA KIKOLONI

Upigaji picha ulikuwa ni silaha kuu mikononi mwa wakoloni. Utawala wa Wajerumani katika Afrika Mashariki ni mfano halisi. Upigaji picha ulitumiwa kuunda picha za mtu binafsi na wengine na kuhalalisha unyonyaji na unyanyasaji wa wakoloni. Kama kanuni ya jumla, picha hizo zilikuwa za ubaguzi wa rangi na dhana potofu.

Watu weusi mara nyingi walioneshwa kwa njia za kudhalilisha na kupigwa picha kinyume na mapenzi yao. Kwa mfano, walioneshwa wakiwa wamebeba watu weupe au wakiwa wamepigwa picha wamevaa minyororo. Tofauti na hilo, watu weupe mara nyingi walijionesha kuwa wenye nguvu na bora zaidi.

Mandhari mara nyingi yalioneshwa kuwa hayana watu, na hivyo kujenga hisia potofu kwamba rasilimali ambazo Milki ya Ujerumani ilitaka kunyonya hazikuwa zikitumiwa na watu na kwamba ardhi ilikuwa imelala. Picha hizo ambazo zilitumika kama propaganda nchini Ujerumani bado zinaunda fikra za leo kuhusu watu weusi na weupe na taswira zetu za jamii za Tanzania na bara la Afrika kwa ujumla.

## MARA NYINGI TUNAFIKIRI KWAMBA UPIGAJI PICHA UNAONESHA „UKWELI“. LAKINI SIYO HIVYO BALI NI UKWELI ULIOUMBWA KWA KUTUMIA PICHA HIYO.





Picha 17

## JE, MPIGA PICHA ALIKUWA NA DHUMUNI GANI WAKATI WA KUPIGA PICHA HII?

## HUONI NINI?



Picha 18

Tujiulize: Je, ninaweza kufahamu nini kuhusu picha hii, watu hawa, maeneo haya?
Picha imegawanyika kama ifuatavyo kwenye kanzidata ya Ethnologisches Museum: Nature photography: (mimea, uoto wa asili) / picha za kikundi (watu) / mazingira, shughuli
Ilichukuliwa kwenye shamba la pamba Saadani Kaskazini-Mashariki mwa Tanzania. Jina la mpiga picha halijatajwa. Picha hiyo huenda ilichukuliwa wakati wa ziara ya mfanyakazi wa benki na katibu wa serikali katika kile kinachojulikana kama "Reichskolonialamt" (Ofisi ya Kifalme ya Kikoloni), Bernhard Dernburg, mnamo mwaka 1907, na labda ilikuwa sehemu ya mfululizo wa kumbukumbu za matumizi ya jembe la mvuke kwenye mashamba ya „Wajerumani". Jirani na Bahari ya Hindi Kaskazini mwa Dar es Salaam na Bagamoyo, Saadani ilikuwa ni kituo muhimu cha biashara Kaskazini-Mashariki mwa Tanzania wakati huo. Leo hii ina takriban wakazi 800 na haiko mbali na Hifadhi ya Kitaifa ya Saadani. Magofu kadhaa yanashuhudia historia yake muhimu.

## KWA NINI MOTIFU NI MUHIMU? KWA NINI HASA MPIGA PICHA ALITAKA KUPIGA PICHA HII?

Pamoja na mpira, pembe za ndovu, na mkonge, kilimo cha pamba kisichotumia maji, kilikusudiwa kuboresha usawa wa kibiashara wa makoloni ya Wajerumani katika Afrika Mashariki ya Mjerumani. Shughuli hizi zilitokana na unyonyaji wa watu na rasilimali. Picha kama hizi zilitumika kutangaza makoloni kama faida kwa uchumi wa Ujerumani na kama soko la bidhaa za Ujerumani, zana za kilimo na usafirishaji wa mizigo.

Picha zinazoonesha utajiri wa kilimo zilitengenezwa kwa kusudi hili, na kujenga hisia kwamba mikoa iliyoathiriwa haikuwa na makazi na haikuwa na kilimo. Walengwa walikuwa ni Wajerumani wenye viwanda na wafanya maamuzi ya kisiasa, na pia hadhira nyingine iliyotakiwa kusadikishwa ni umma wa Wajerumani ili kuonesha faida / thamani ya „mradi wa kikoloni".



## NI NANI ANAYEONEKANA KWENYE PICHA? WANAFANYA NINI? WALIOMBWA RIDHAA YAO?

Makampuni binafsi yalifaidika na makoloni, lakini ilikuwa ni hasara kwa serikali ya Ujerumani, na faida iliyotarajiwa haikupatikana. Serikali ya kikoloni ya Afrika Mashariki ya Mjerumani ilipitisha hatua mbili za kulazimisha watu kufanya kazi mashambani: kwanza, kwa kulipa kodi iliyotozwa katika kila nyumba ambapo mtu angelipwa kwa njia ya kufanywa kibarua.

Watu wa Afrika Mashariki walipinga. Kwa kukataa kufanya kazi walisababisha ucheleweshaji, kodi haikupatikana: kuanzia mwaka 1905 na kuendelea, kila mtu mzima alipaswa kufanya kazi fulani kwenye shamba la mkoloni au kulipa fedha sawa na kazi ambayo angefanya. Kwa hiyo, watu walizidi kuwa na muda mdogo wa kufanya kazi katika mashamba yao wenyewe.

Picha hii ilikusudiwa kuonesha umma wa Wajerumani kuwa koloni la Afrika Mashariki ya Ujerumani lilitoa ardhi yenye rutuba na wafanyakazi.

## HADITHI GANI ZA KIKANDAMIZAJI NA ZILIZOPUUZWA ZIMEFICHWA HAPA? NI NINI KINACHOBAKI HAKIONEKANI? UNAONA NINI?




Picha 19

Watu walioishi katika eneo la Tanzania ya sasa walipinga utawala wa Wajerumani na unyonyaji tangu mwanzoni. Aina mpya ya upinzani iliibuka Kusini mwa Tanzania mwaka 1905, wakati jamii kadhaa zilipokutana kwa mara ya kwanza na kuvuka mipaka ya maeneo yao ya kisiasa. Vita vya Maji Maji vilianza kipindi watu walipoharibu shamba la pamba la „Wajerumani" huko Nandete (Kusini mwa Tanzania ya sasa) ili kupinga mfumo wa unyonyaji wa kodi. Kwa kuchochewa na wito wa kinabii dhidi ya upinzani na dhana ya kinga ya kiimani iliyojulikana kama – maji – majeshi yaliingia vitani kusini mwa Tanzania dhidi ya nguvu ya koloni la Kijerumani.

Picha hii ni ya shamba la pamba likiwa na wafanyakazi (ilipigwa mnamo mwaka 1907) ni wakati ambao jeshi la kikoloni la Wajerumani liliwakandamiza wapiganaji na wapinzani wao kwa ukatili wa hali ya juu. Takriban watu 300,000 waliuliwa au walikufa kutokana na madhara ya uharibifu wa makusudi wa maisha yao.







NJIA:

Picha za kikoloni zilipigwa bila kujali haki. Watu wanaoonekana kwenye picha hizi inaonesha hawakuombwa ridhaa yao, na mara nyingi wanaoneshwa katika namna ya kudhalilishwa. Picha zilitumika kwa ajili ya maslahi ya dola, na ndiyo maana inabidi kuzishughulikia hizi picha kwa umakini mkubwa na tahadhali. Katika maonesho haya, picha ya shamba la pamba inaonesha imepigwa kwenye mapaneli ya pamba (angalia picha namba 18). Hii inatokana na kipande, picha kamili inaweza kuonekana kama hivyo. Hawa wageni hawakuishia tu kupiga picha zinazoonesha hayo bali pia waliweza kuzipiga kupitia usanikishaji. Kipande hiki kinatupatia fursa ya kuibua huu mjadala kuhusu eneo la kazi na inafanya tupingane na hoja kwamba waliopigwa picha waliridhia kutokana na muktadha wenyewe unavyoonekana.










Picha 20 – 23



## KUULIZA MASWALI NA KUJENGA TASWIRA (YA DUNIA)

Je, picha ya "safari" ina uhusiano wowote na ukoloni? Wakati wa enzi za utawala wa kikoloni, picha zilitumiwa na mamlaka kama silaha muhimu ya kiutawala. Kwa mfano, mtu Mweusi alionekana hajavaa nguo kwa ajili ya kuwadhalilisha, wakati watu weupe walionekana kwenye pozi za kimamlaka. Kwa ajili ya malengo ya kipropaganda, ardhi ilikuwa inaonekana haikaliwi na pia ilikuwa na rasilimali tele.

Hata hivi leo, matamanio ya kikoloni yanaakisiwa kupitia sanaa na vyombo vya habari; na kwa kupitia picha, magazeti, na filamu ili kuendeleza mtazamo wetu kuhusu dunia. Warsha ya "Dunia (Taswira): Kuzisoma Picha za Kikoloni" inagusia na inatathmini ni kwa vipi matamanio ya kikoloni bado yanavutia wapigapicha na waandishi wa magazeti wa hivi leo?

Katika warsha, kikundi cha wanafunzi kilitengeneza "zinezi", yaani kigazeti kidogo cha kukunjwa. Kwa kutumia mbinu ya kolage, walitumia picha za kihistoria na za kisasa ili kutengeneza dunia mpya ya kijigiti ambayo inaruhusu mtazamo hakikifu wa ukoloni na picha za kikoloni. Hiyo zinezi iliyoundwa ilijumuishwa kwenye maonesho na baada ya kila warsha, ilikuwa ni kazi ya ziada maana kila shubaka likawa limejaa hizi nyaraka zikiakisi mtazamo wa kizazi kipya.

## NOTSI ZANGU

## NJIA: FIKRA MUHIMU

Kwenye meza ya maonesho, wageni waliweza kuona picha za kikoloni “Unter den Akazien” (Chini ya mti wa mshita) na ikawekwa foili fulani inayoakisi kuhusu picha hiyo. Kila foili inayoakisi ikaongeza thamani kwenye mchoro na kuibua maswali kwenye hizo picha, ikiangazia ukweli kwamba picha daima huweka mtazamo *mmoja* wa ulimwengu ambao kwa hakika unachaguliwa na mpigapicha. Wageni walishawishiwa kuuliza maswali kuhusiana na kilichooneshwa kama vile malengo ya mpigapicha yalikuwa ni yepi alipopiga picha. Pia walichangamshwa kwa kutakiwa wafikirie ni nini kinaweza kuwa kimeachwa kwenye picha hiyo. Kwa mfano, je ni kitu gani kimefichwa na picha au nyuma ya mpigapicha?





Picha 24




Picha 25

## NOTSI ZANGU

## JE, WATU WALIFAHAMU KWAMBA WANAPIGWA PICHA?

## JE, NI BENDERA GANI INAONEKANA PICHANI?



## JE, HUO MJI NYUMA YA HIYO PICHA UNAONEKANAJE?

# NYARAKA ZA KIKOLONI NA MAPENGO YALIYOPO

Nyaraka ni sehemu ya kuweka hazina ya ushuhuda wa mambo yaliyopita. Uchaguzi wa nyaraka na namna zilivyopangwa inaakisi, pamoja na mambo mengine, mitazamo fulani ya kidunia na maslahi ya kimamlaka. Kwa kutumia vitu halisi pamoja na taarifa zote zilizoandikwa, makumbusho pia ni aina  fulani ya nyaraka. Lakini ni nani anayeamua kwamba hadithi fulani ikumbukwe na hadithi ipi ipuuzwe? Nani anayeamua nyaraka zipi zitambuliwe Ulaya na zipi zichukuliwe kwamba hazina maana yoyote? Makumbusho yanaakisi mpangilio wa dunia ya kikoloni na ya kibaguzi ya karne ya kumi na nane. Vitu vinavyoonesha “sanaa” na “historia” ya Ulaya vilikusanywa kwenye makumbusho mahususi. Kinyume chake sanaa na vitu vya kitamaduni kutoka Asia, Afrika, Amerika, Oceania, na Australia vilishushwa thamani kwamba ni “ethnografika” na vyanzo vyake na hizo jamii vikaitwa “visivyo na sanaa” na “visivyo na historia”.




Makumbusho ya The Königliches Museum für Völkerkunde (Makumbusho ya Kifalme ya Ethnolojia) ambayo ilifunguliwa mwaka 1886, inaonekana kuwa na vitu mbalimbali vya kisanaa. Kwa namna hiyo wafanyakazi kwenye makumbusho haya wanawasiliana na wafanyakazi wengine duniani kote na wameendelea kutunza mahusiano mazuri kati yao na wanajeshi, masetla, wamisionari na watafiti katika maeneo yaliyotawaliwa. Katika Azimio la Federal Council (Bundesrat) la mwaka 1889 liliamuru makumbusho ziwe “sehemu ya kukusanyia” vitu vilivyojulikana kama “vitu vya kiethnolojia” kutoka kwenye makoloni. Wanaethnolojia wa Berlin walitumia nguvu (kwa kuiba, kurubuni, kutumia vita n.k) ili kuvipata vitu hivyo. Hata hivyo wazimu huo wa kukusanya ulimaanisha kwamba makumbusho baada ya muda mfupi yangefurika kutokana na jukumu la kuvidhibiti na kuviweka vitu hivyo kwenye nyaraka.

Siyo vitu vyote vilivyochukuliwa na majeshi ya kikoloni ya Mjerumani vilifikishwa kwenye makumbusho. Mamia ya kampeni za kijeshi yanadaiwa kupoteza maisha ya watu wasiohesabika. Majeshi ya wakoloni yalipora ng’ombe na pembe za ndovu na kuharibu nyumba na mashamba. Ilipofikia wakati wa Wajerumani kunyanyua mikono juu (kuachilia) Afrika Mashariki ya Ujerumani baada ya Vita vya I vya Dunia, wakaharibu baadhi ya nyaraka za utawala wa kikoloni, ikiwemo karatasi walizonyang’anywa viongozi wa kijamii. Baada ya Vita vya II vya Dunia, Jeshi la Kijamaa likasafirisha vitu walivyovichukua kwa – jina la kukusanya vitu kwa ajili ya makumbusho ya Berliner Museum für Völkerkunde kwa ajili ya Muungano wa Ujamaa. Kiasi kikubwa cha vitu hivi kilirudishwa Berlin baada ya kuanguka kwa ukuta wa Berlin. Vitu vingine ambavyo pia “vilichukuliwa”– kama vile kadi za indeksi za vitu vya Waafrika – viliharibiwa wakati wa vita. Vitu muhimu vimerekodiwa kwenye orodha ya makumbusho havijahesabiwa na inachulukuliwa hii leo kwamba “vimepotea”.

## NINI HAKIKUCHUKULIWA?

Ingawaje kumilikiwa kwa vitu na Ethnologisches Museum Berlin inadai kwamba inawakilisha utamaduni “asilia”, kinachofanyika ni kuzalisha taarifa za uongo, za kikoloni na zenye taswira ya kibaguzi zenye ubaguzi wa rangi wa historia za jamii zisizobadilika. Vitu ambavyo haviendani na ubaguzi huu hazikuwekwa katika makumbusho hizi.

Afrika ya Mashariki imeshiriki katika soko la dunia la kibepari tangu karne ya kumi na tisa, ikiingiza vitu mbalimbali kutoka Asia, Ulaya na Amerika, vikiwemo vitambaa, nguo, shaba, na shanga za kioo. Vitu vya anasa kama vioo vya Ufaransa na shampeni navyo vilikuwepo. Cha muhimu zaidi aina mbalimbali ya bunduki ziliingizwa zikitokea Ulaya. Kwa muda mrefu, mahusiano na mawasiliano ya kikanda na kidunia yaliyokuwa yanazingatiwa na jamii za Kiafrika yalipuuzwa na kufanywa yasijulikane kupitia historia ya Ulaya na kupitia sera ya “ukusanyaji” ya makumbusho.



Picha 26

Mwanzoni mwa utawala wa kikoloni katika Afrika ya Mashariki, watendaji kama vile Mirambo mmiliki wa kiko, walikuwa na nguvu sana kuliko watendaji kama vile Hermann von Wissmann, ambao walikuwa wamejilimbikizia vitu, walijiona wao ni bora kupita kiasi. Wissmann na msafara wake hawakuwa na kitu chochote kwa mara ya kwanza alipokutana na Mirambo mwanzoni mwa miaka ya 1880. Mtawala akawasaidia kwa kuwapa pesa na vitu kwa ajili ya biashara ya kubadilishana vitu. Kama ishara ya upendo, Mirambo akampa Wissmann kiko chake.

Zawadi za ukarimu za Mirambo zilizosaidia kumtoa Wissmann kwenye "mazingira ya kufedheheka", zinathibitisha tabia ya kujiamini ya mfadhili ambayo alidhania anayo Wissmann. Siyo kiko cha bakuli pekee, lakini pia si chupa za shampeni au bunduki za Mirambo pekee, vyote hivyo viliishia kumilikiwa na jumba la makumbusho huko Berlin. Mahusiano makubwa ya kibiashara ya Mirambo yalifanywa yasionekane wakati wa kuporwa na wanaethnolojia wa Berlin, na pia mali za kisasa na kihistoria za kikanda na kimataifa za jamii za Kiafrika Mashariki.

Mtyela Kasanda, ambaye pia anajulikana kama Mirambo (c. 1840–1884), alikuwa ni kiongozi mashuhuri wa Unyamwezi. Cheo chake ni Mtemi. Alitawala eneo kubwa sana kuanzia Ziwa Viktoria hadi katikati ya Tanzania mpaka Ziwa Tanganyika. Pia alimiliki misafara kadhaa ya biashara na akauimarisha utawala wake kwa kufanya biashara zilizomnufaisha, hasa ikiwa ni pembe za ndovu. Mirambo alinunua bunduki, risasi na vitu vingine. Askari wake waliendelea – kuogopwa Waruga-ruga – ndio waliolinda himaya yake.

Hermann von Wissmann (1853–1905) alikuwa ni mmojawapo wa wanajeshi wa Kijerumani. Alichora ramani ya maeneo mbalimbali ya Afrika kwa ajili ya utawala wa watu wa Ulaya, akakusanya askari wa Kiafrika na kuanzisha Jeshi la kikoloni chini ya kamanda wa Kijerumani ambaye alitaka kwa nguvu aanzishe Dola ya Kijerumani kwa kutumia wasomi wa kisiasa na kiuchumi wa Afrika ya Mashariki. Jamii zilitoa upinzani mkali. Wissmann pia alijulikana kama Gavana wa Afrika Mashariki ya Ujerumani mwaka 1895/96.




„Mirambo alinipa ndama mzuri na chupa mbili za shapeni kama sijakosea ni Pomery & Greno kama zawadi ya ukaribisho. […] Watu wangu walinilalamikia kwamba hawawezi kununua kitu chochote hapa kwa kutumia shanga walizokuwa nazo, kwa kuwa watu walikuwa wakihitaji nguo. Na kwa kuwa sikuwa na vitambaa, nilimwelezea Mirambo aibu hiyo iliyonipata. Mara akaagiza nyumbani mwake watoe majora manne ya vitambaa yenye urefu wa mita 40 kila moja yakaletwa na nikakabidhiwa. Nikauliza kama ninaweza kumlipa kiasi cha dola senti 32 huko Tabora, lakini akasema hana mawasiliano yoyote huko wala sehemu yoyote na akaniomba niipokee hiyo zawadi yake ndogo. Pia akaniongezea na mishale, mabakuli na ngao kutoka kwenye kiwanda chake cha silaha pamoja na kiko alichokitengeza yeye mwenyewe pamoja na bakuli lililotengenezwa kutokana na jiwe la sabuni ambalo liko upande wa Kaskazini kutokea hapa."

Hermann von Wissmann, *Unter deutscher Flagge quer durch Afrika von West nach Ost*, Berlin, 1889.

„Ili kurudisha fadhila kutokana na zawadi nyingi nilizopewa na kama asante ya urafiki nilioupata mahali hapa, nilimpa Mirambo bunduki pamoja na Pogge aliyoniachia. Mirambo akaniambia kwamba hataki kuniaminisha kwamba amenisaidia kwa hicho kitu kidogo alichonipa bali angekubali bunduki kama ishara ya urafiki."

Hermann von Wissmann, *Unter deutscher Flagge quer durch Afrika von West nach Ost*, Berlin, 1889.




Picha 27

## NI KWA VIPI KITU AMBACHO “HAKIPO” KINAWEZA KURUDISHWA?

## NOTSI ZANGU

**Ethnologisches Museum**
Staatliche Museen zu Berlin

*Maelezo ya kitu*
**Kiko cha tumbaku**

*Kichwa*

*Namba ya utambulisho*
**III E 1564**

*Sehemu ya maonyesho*
**242.2.6.1.2. Silaha za moto**



. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Rejea ya kijiografia*
Tanzania
Data ya kihistoria (katalogi kuu) Unyamwesi (Unyamwezi)

*Binafsi/Umma*
Mkusanyaji: Hermann von Wissmann (4.9.1853 - 15.6.1905)
Mmiliki wa awali: Mirambo (Mytela Kasanda) (ca. 1840 - 1884)

*Vipimo*
11,2 x 14 x 5,8 cm
< 2 kg

*Malighafi/Teknolojia*
Malighafi: jiwe (jiwesabuni)

*Hali*
1. Isiyo na ukosoaji/nzuri (03.03.2015)

*Maelezo mafupi*
Maelezo mafupi: katalogi kuu: "tumbaku=kiko cha tumbaku kilichotengenezwa kwa jiwe na Mirambo. Unyamwezi. Urefu sm 14 "

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Ufafanuzi*
Umbo: Bakuli ndogo ya koni yenye mdomo mpana wenye umbo la faneli.
Goti kali. Pua ya bomba yenye bega bapa iliyo na shanga (kama vile mianzi)
Rangi: Kijani cha krayoni
Hali ya uhifadhi: vipande vidogo vinakosekana

*Uainishaji*
. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Numba nyinginezo*
Mkusanyaji na.: 131

*Mmiliki wa awali*
. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Tarehe ilipochukuliwa*
1883

*Maoni*
[redacted]

HK ilihakikiwa [HeOr], rejea ya kijiografia ilihakikiwa [PI]

Picha 28

Je, itachukua muda gani kutafsiri maelezo ya Kijerumani ya zaidi ya vitu milioni moja vilivyohifadhiwa katika kanzidata ya Makumbusho ya Ethnolojia katika lugha za Kiingereza au nyinginezo?

*Watu wote*

Je, Mirambo alikiitaje kiko?
Je, kwa Kinyamwezi kitu hicho kiliitwaje?

*Kristin*

Ni kategoria zipi zimepuuzwa hapa au kusahauliwa?

*Jocelyne*

Kwa kawaida majina ya watu wa Afrika Mashariki hayatajwi.
Je, ni kwa nini Mirambo anatajwa?

*Paola*

Je, hiki kitu kilitumika? Je, kiko kilikuwa na umuhimu gani kwa Mirambo?
Je, haya maelezo yanayotolewa yanamsaidia nani kuelewa?

*Jocelyne*



## NJIA: "KUSOMA KWA JICHO YAKINIFU NA KUELEWA HISIA ZA MTUNZI"

Ni nani anayeamua usimuliaji wa historia, ukweli unakumbukwa, na mitazamo gani inaonekana? Watu wanaotengeneza nyaraka ndiyo wanaoidhibiti simulizi inayotolewa. Maneno yanayotumika na kategoria za kwenye kanzidata kama istilahi "mmiliki wa zamani" na "mkusanyaji" hayafanani, jambo linalofanya zilete utatanishi. Taarifa kuhusu umuhimu na dhima ya kuonekana mali za kitamaduni hazipo. Hata hivyo, hatuwezi kufahamu ni kwa vipi watu wa Afrika Mashariki waliutafsiri uporaji uliofanywa na wakoloni wa Ulaya. Taarifa za kwenye kanzidata ya makumbusho zinakumbwa na kitendawili cha kutokuwepo, kategoria za Kiulaya,  na pia taarifa zilizopo zimepotoshwa usahihi wake. Ili kutoa mazingira ya kusoma kwa umakinifu na tahadhali nyaraka zinazojulikana kama "kinyume na nafaka" yaani kusoma kiyakinifu na kuangalia "katikati ya mistari" ikimaanisha kusoma hisia za mtunzi, baadhi ya taarifa zinazowasilishwa kwenye maonesho zimewekewa rangi ya pinki. Mfano mzuri wa taarifa hizo zilizopo katika makumbusho – ni inayohusu "kiko bakuli cha tumbaku" (angalia picha namba 28) – ambacho kimeambatanishwa na kitufe chenye kauli zinazoibua maswali: Je, neno "mkusanyaji" linamaanisha nini? Je, hili eneo lililotajwa ni sahihi? Je, ni kategoria zipi zilipuuzwa au kusahaulika? Nani anaamua 'vitu' ziwekwe kwenye kategoria fulani?

Maonesho ya *Kuonyesha.Kutokuwepo* yalijumuisha vipengele mbalimbali vya ushiriki na kimojawapo ni “mchoro wa kamba”. Mchoro unawakaribisha wageni kuangalia makavazi ya "kila siku" kwa umakini na kutandaza kamba kwenye majibu sahihi. je, makavazi ni nini? je, unakutana na makavazi ya aina gani?

1. Chukua kalamu.

2. Anzia pa kuanzia.

3. Ukianzia kushoto kwenda kulia: Soma maswali, chagua majibu sahihi, kisha chora mstari kuzungushia majibu yako.

PA KUANZIA

MIMI NI ...
UMRI WA MIAKA ...

- < 75
- 71–75
- 66–70
- 61–65
- 56–60
- 51–55
- 46–50
- 41–45
- 36–40
- 31–35
- 26–30
- 21–25
- 16–20
- 11–15
- > 10

TAYARI NILISHATEMBELEA HUMBOLDT FORUM.

- Ndiyo
- Hapana

| MAKAVAZI MBALIMBALI YANAWEZA KUTUMIKA YA AINA TOFAUTI. NINAZOZIPENDA ZAIDI ... | NINAFIKIRIA MAKAVAZI HII ... | NINAFIKIRIA MAKAVAZI HII ... |
|---|---|---|
| Kuandika & kusoma shajala | | Zimepangiliwa vizuri |
| Kusoma maktaba | | Zina upendeleo |
| Kuzungumza na wazazi / babu na bibi / watu wazima | | Kila wakati zinabadilika |
| Kuperuzi kwenye mtandao wa intaneti | Ziko kati haziegemei popote | Zimepangiliwa vizuri |
| Kusoma kanzidata na nyaraka | | Hazitendi haki |
| Kusikiliza muziki na mazungumzo | | Hazina upendeleo |
| Kuangalia filamu za makala (dokyumentari) & filamu | | Zina hisia |
| Kwenda makumbusho & kwenye maonesho | Ni binafsi | Zina upendeleo |
| Kutembelea maeneo ya kumbukumbu | | Kusanya nyingi |
| Kutaangalia nyaraka za zamani na albamu za picha za familia za wazee | | Zina haki |
| Makavazi ambayo haijatajwa hapa | | Inaonesha tu sehemu ya picha |



MWISHO

Abb. 29

# VITU – KUANGALIA UPYA


Vitu vimewekwa katika uhusiano na mwingiliano wa wanadamu. Katika onyesho la vitu hivi unaweza kuona mbadala wa vitu vinne. Tunapenda kukuambia sehemu ya hadithi zao ambazo zinajulikana kwetu: kuhusu watu waliotumia vitu, kuhusu jukumu la vitu katika jamii zao husika, na kuhusu matukio ya kikatili ambayo wamiliki wa mwanzo na vitu vyao waliyapitia.

Tunafanyaje – timu ya maafisa waangalizi weupe – wanafahamu hadithi hizi ndogondogo? Tulizipata kwa kutafuta kwenye kumbukumbu za kikoloni, ambazo zina taarifa fulani, lakini pia zina mapungufu mengi na zinasisitiza chuki na ubaguzi wa rangi, na tulijaribu kusoma kumbukumbu hizi katika njia zisizofahamika na kwa umakini. Hii ndiyo sababu nafasi za pinki katika sehemu hii ya maonesho inaashiria nafasi zilizo wazi – na hivyo kuangazia vikwazo vya kumbukumbu zetu na mtazamo wetu kuhusu vitu vitatu kati ya vinne vilivyochukuliwa kwa njia ya kikatili. Hatufahamu kama watu kutoka kwenye nchi zao na maeneo ya asili wangekubali jinsi ambavyo vitu hivi vingewasilishwa leo. Kwa upande wa kitu cha nne, hatufahamu kama mmiliki wa awali alikubali kionyeshwe kwenye Jumba la Makumbusho. Hii ndiyo sababu hatuonyeshi vitu asilia, bali tunaonyesha mbadala.



## NJIA:
## KUWARUHUSU WARITHI KUELEZEA

Kwa kuzingatia msingi ambao maonesho haya unaufuata, ambao ni “Hakuna Idhini – Hakuna Kitu?”, vitu asilia ni miongoni mwa hivi ‘vitu’ vinne kwenye maonesho haya havikuonyeshwa. Hata hivyo, ili kusimulia hadithi zao, michoro ya 3D, michoro ya kisanaa, au dondoo ya hivi ‘vitu’ viliwawasilishwa. Kwa mfano, michoro myeupe ya 3D za *kigiilya* zilionyeshwa zina alama za vidonda vilivyowekewa rangi ya pinki (angalia picha namba 36). Hivyo, kitu asilia hakikuonyeshwa kwa sababu hakukuwa na ridhaa iliyokuwa imetolewa, lakini nakala yake ilionyesha ni simulizi ya kikatili inayohusiana na sanamu hiyo. Mkabala huu unafanya kuwe na heshima na kuzingatia unyeti wa kuwasilisha vitu vya kitamaduni kwenye maonesho ambayo yataibua mjadala.



## NOTSI ZANGU

## *KIGIILYA.*
## NI SANAMU NDOGO YA BINADAMU YA MBAO KUTOKA KISIWA CHA BUKEREBE KATIKA ZIWA VIKTORIA.



Picha 35

Takwimu za ukatili ziliandikwa, kama alama inavyoonyesha. *Kigiilya* iliporwa, kuonyeshwa na kuharibiwa katika muktadha wa kidhalimu wa kikoloni. Takwimu hizo zimeunganishwa kwa njia maalumu na uhusiano wa kiutawala kabla na baada ya utawala wa kikoloni. Washirika wengi wamehusishwa nayo: *bakama* (wafalme) wa Bukerebe na mababu zao, wasomi wa kisiasa, misafara ya wafanyabiashara wa Kinyamwezi, Wamisionari wa Kikatoliki na Makatekista wa Afrika Mashariki, wanajeshi wa Ujerumani, wapelelezi (kama washiriki wa wavamizi wa kikoloni) na wafanyakazi wa Jumba la Makumbusho la Museum für Völkerkunde huko Berlin (Makumbusho la Ethnolojia Berlin) pamoja na mwandishi Mtanzania Aniceti Kitereza, mjukuu wa *omukama* Machunda, na wengine wengi.



## NI KITU AU KIUMBE?

— Mnamo mwaka 1895, jeshi la kikoloni la Ujerumani lilipigana vita dhidi ya *omukama* (mtawala) wa Rukonge, wafuasi wake na wakazi wa kisiwa cha Bukerebe katika Ziwa Viktoria. Wanajeshi wa Kijerumani walipora picha, ambayo ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Rukonge.

Ilionyeshwa katika kituo cha wamisionari wa kikatoliki cha White Fathers huko Bukerebe. Kundi la waumini walipiga picha hiyo kwa fimbo na kuikata kata. Yamkini, lengo lilikuwa ni kuwadhihirishia wakazi wa kisiwa cha Bukerebe kwamba mtawala wao hakuwa na nguvu tena. Mwaka 1997, Luteni Paul Kollmann aliidhinisha sanamu ndogo iliyoharibiwa sana na „kukabidhi" *kigiilya* kilichoporwa kwenye Makumbusho ya Kifalme ya Ethnolojia (Ethnologisches Museum Berlin) mwaka huohuo.

— *Kigiilya* ilikuwa ni ishara ya mamlaka ya *omukama* Rukonge, ambaye alitawala kuanzia mwaka 1870 na kuendelea. Mrithi wake na baba Machunda, ambaye alikuwa anaheshimika kama mleta mvua, inadaiwa alipata hiyo karama kutoka kwa Mnyamwezi asiyejulikana. Msanii aliyekuja kwenye msafara kutokea Tabora alitengeneza uchongaji huo ili kuonesha enzi zake huko Bukerebe. Mjomba wa Machunda Kinabo alifariki siku ambayo kilikamikishwa kutengenezwa, na kulingana na simulizi, Machunda alihamishi roho yake kwenye kinyago ili kuonesha nguvu zake. Pia mwanawe Rukonge alitumia kinyago hicho kuwaonesha washauri wake, Wakerebe wa ngazi za juu, na wageni muhimu ili kuonesha nguvu zake. Rukonge alikitunza *kigiily*a katika nyumba yake binafsi ya kulala *(naruzwi)*, na kilikuwa kikilindwa na walinzi wa kike Muzubwa.



Picha 36

## JE, *KIGIILYA* KINA NGUVU?

## JE, WIZI HUO ULIACHA PENGO GANI? MMLIKAJI ALIKUWA NANI?

„Je, itakuwaje, kama ilikuwa ni ishara ya mapatano, Wajerumani wangekuja kisiwani na kunisaidia kujenga upya ikulu kongwe, Bukindo Nkokoro, ikulu ya Mfalme Rukonge na mizimu yake na kuifanya iwe ni makumbusho. Ili kwamba kigiilya arudishwe kwao salama salmini. Na kwa kufanya hivyo, familia zetu za wafalme wetu wa hapo kale hatimaye watapumzika kwa amani.“

*Omukama* Talengwa Kaseza Lukumbuzya in Berlin, Juni 2023, Übersetzung in Deutsche von Silke Körber, Berlin, 2024.



## KWA NINI SANAMU NDOGO ILIITWA *KIGIILYA*?

— *kigiilya* · Tanzania, Bukerebe (Ukerewe) · Karne ya 19. · Mbao · cm 114 × 31 × 16.5 · watengenezaji, watumiaji, walinzi, wamiliki: msanii asiyejulikana wa Katikati ya Tanzania (Mnyamwezi?); *omukama* Melango Buyanza Machunda mpaka 1870; Muhase Itugara Rukonge; Muzubwa, mwanachama wa kikundi cha ukoo wa Abazubwa, mpaka mwaka 1895; askari wa jeshi la kikoloni la Wajerumani mpaka mwaka 1895/1896(?); wamisionari na makatekista wa White Fathers (Pères Blancs) mpaka mwaka 1897; Paul Kollmann mpaka mwaka 1897; kuanzia mwaka 1897 Jumba la Makumbusho la Königliches Museum für Völkerkunde, Berlin (Ethnologisches Museum, Staatliche Museen zu Berlin, III E 5529).

— Mwaka 2023, *Omukama* Talengwa Kaseza Lukumbuzya, kizalia wa *Omukama* Rukonge, alitumia siku tatu kutembelea hifadhi ya mali za Ethnologisches Museum Berlin in Berlin katika wilaya ya Dahlem na warsha mbili za maonesho huko Humboldt Forum. Pamoja na vitu vingine vya nyongeza ambavyo ni vya kitamaduni kutoka Bukerebe ambavyo vilichukuliwa kutoka kwenye makabati ya kuhifadhia vitu. Lengo kuu la maonesho haya likiwa ni kwenye sanamu ya binadamu inayojulikana kama *kigiilya*. Tulizungumza na Omukama kuhusu sanamu hii na mali zingine za kitamaduni huko kwenye hifadhi ya Ethnologisches Museum na kuelewa kuwa ni ishara na matumizi ya ishara hiyo kwa Wakerebe.

# MFUKO WENYE VIFAA VYA DAWA



Picha 37

Mfuko huu wenye vifaa 96 vya dawa vinatuambia mambo mengi tofauti. Kwanza kabisa, inatuelezea hali ya kijamii ya waganga muhimu katika Afrika Mashariki walikuwa na nani wakati huo. Wawakilishi wa serikali ya kikoloni ya Kijerumani waliwaona waganga kama watu muhimu walio na upinzani mkali wakati wa vita vya Maji Maji hivyo waliwakamata na kuwaua. Pili, mfuko huu unaashiria ujanja wa ukusanyaji usiofaa wa wataalamu wa Ethnolojia wa Berlin, ambao walifuata kama washirika wa jeshi la Kijerumani. Vita vya Kikoloni vilichukua nafasi kubwa katika ugawaji wa vitu.

Mfuko huu, ambao ulikuwa umesahaulika katika bohari ya Makumbusho zaidi ya karne moja iliyopita uliaminika kuwa umepotea, umejaa taarifa kuhusu mbinu za kitabibu ambazo bado zinajulikana kwa waganga wa kisasa. Mnamo mwaka 2017, huko Mohoro wakati wa safari ya kitafiti ya wanasayansi na wasanii wa Kitanzania, waganga walishirikisha maarifa yao kuhusiana na baadhi ya vitu hivyo. Mfuko huu na vyote vilivyomo ndani yake ni vitu nyeti ambavyo awali vilikusudiwa kutumiwa na waganga pekee na havikupaswa kuonyeshwa hadharani. Inaonesha kuwa mfuko huu ulipatikana kwa njia ya kidhalimu. Hivyo, unawasilishwa hapa kupitia mchoro uliochorwa na msanii wa Kitanzania Amani Abeid.



— Historia ya mfuko wenye vifaa vya dawa imehusishwa na upinzani wa wakazi wa Afrika Mashariki wakati wa vita vya Maji Maji (1905–1907). Mmiliki wake wa awali alikuwa ni mganga kutoka Kusini mwa Tanzania. Mmoja wa waganga hao ambaye jina lake linafahamika ni Kinjeketile Ngwale (pia anajulikana kama Kinjikitile), ambaye alikuwa kinara wa vita vya Maji Maji kupitia utabiri wake wa kuandaa maji matakatifu *(maji)*. Mnamo mwaka 1905 aliwindwa na jeshi la kikoloni la Wajerumani, akachukuliwa kama mfungwa na hatimaye (pengine mwaka huohuo) aliuawa huko Mohoro, ambapo mfuko huu wa dawa ulikuja kumilikiwa na Wajerumani. Mnamo mwaka 1907, mgawanyiko wa kikoloni wa Ofisi ya Kigeni ya Ujerumani ulituma mfuko huu kwenye Jumba la makumbusho la Museum für Völkerkunde huko Berlin (Ethnologisches Museum Berlin) kama "nyara za kivita". Uliingizwa kwenye orodha kuu ya kihistoria yenye maelezo ya kibaguzi, na yenye kudhalilisha "Gunia lililotengenezwa kwa ngozi ya mnyama pamoja na vyombo vya kichawi."

— Kuanzia miaka ya 1960 na kuendelea, wanasiasa na wanasayansi katika Tanzania huru, walikuwa wakivionesha Vita vya Maji Maji kama chanzo cha harakati za kupigania uhuru wakichochea umoja na mshikamano miongoni mwa watu wa mikoa mbalimbali ili wajiunge katika vita hivyo. Rais Julius Nyerere na chama chake cha TANU kikawezesha mshikamano miongoni mwa wananchi ili kutekeleza malengo ya sera za Ujamaa wa Kiafrika *(Ujamaa)*.

Matokeo yake, masuala kama vile ushirikiano na Wajerumani na maslahi ya madola mbalimbali yanayopigana yalipuuzwa wakati wa kutathmini upya matukio ya Vita vya Maji Maji. Hata hivyo, vita hii ilikuwa ni chachu ya kufanyika kwa tafiti siyo tu za kihistoria, bali pia sanaa za maonesho za Tanzania. Tamthiliya ya kihistoria ya Ebrahim Hussein *Kinjeketile* (1969) ni kazi inayojulikana kimataifa na ilichapishwa huko Ujerumani Mashariki.




Picha 38



— Mfuko wenye vifaa vya dawa · Tanzania, Mohoro (Muhoro) · Pembe, mbao, raffia, glasi, mianzi, ngozi ya mnyama, gamba la kibuyu, mafuta, nyuzinyuzi za mimea, mifupa, n.k. · sm 40 × 20 × 26 (begi) · Mmiliki wa awali/wamiliki wa awali: Mganga, jina halijulikani; Nyara kutoka katika Vita vya Maji Maji; Serikali ya Kifalme ya Kijerumani Afrika Mashariki mwaka 1907 (Kaiserliches Gouvernement für Deutsch-Ostafrika); kuanzia mwaka 1907 yalikuwa yakimilikiwa na Jumba la Makumbusho la Königliches Museum für Völkerkunde, Berlin (Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, III E 14793)

## KWA NINI MFUKO ULIFUNGULIWA?

## JE, KUSUDI LA DAWA KWENYE MFUKO LILIKUWA NINI?




Pichu 39



Picha 40

Ingawa kiti hiki ni kitu kinachojulikana (ikilinganishwa na vitu vingine kutoka Tanzania), maswali mengi bado hayajajibiwa. Hata hivyo, haifahamiki ni nani aliyekimiliki, na tunaweza kutoa dhana zisizowazi kuhusu utambulisho wake. Mwanajeshi wa kikoloni Grawert alimuelezea "sultana" wa Urugu. Jina alilompatia lilionesha ni namna gani washirika wachache wa kikoloni walifahamu kuhusu muundo wa jamii za Afrika Mashariki, ambao kwa kiasi kikubwa ulipuuzwa. Kwa mfano, walitumia vyeo ambavyo vilikuwa vya kawaida kwenye jamii za watu wa Pwani.

Kwa mfano, kama wanawake wa Afrika Mashariki, wangekuwa na kiwango cha juu cha uhuru kama wanawake wa Ulaya, katika suala la uhuru wa kutembea, udhibiti wa miili yao na umuhimu wao kwenye kisiasa – hii ingesaidia kupinga nafasi ya wakoloni. Utawala wa kikoloni na miundo yake ilidhoofisha nafasi ya mwanamke wa Afrika Mashariki, Kijamii na Kiuchumi. Kiti hiki – na ukosefu wa taarifa kuhusu mwanamke aliyekimiliki – ni kielelezo cha ukimya mkubwa unaowafunika wanawake wa Afrika Mashariki katika nafasi za madaraka.



## MWANAMKE HUYU ALIKUWA NANI?

— Yeyote atakayetazama kiti hiki cha kuvutia kutoka Buruku katika bohari ya Ethnologisches Museum hii leo ataona alama ndogo iliyoambatishwa kwa uzi na yenye maelezo "kiti cha mkuu". Neno hilo, ambalo limetumika kwenye kiti kwa miongo mingi linadhalilisha na linatoa taswira potofu ya miundo ya kisiasa. Ukiweka kando lebo yenye matatizo, inapuuzia pia ukweli kwamba hati za awali na maingizo ya katalogi yanataja mwanamke mashuhuri kama mmiliki wa kiti hicho, na vitu vingine vilivyoidhinishwa.

Katika miaka ya 124 ambayo kiti hiki kimekuwa kikimilikiwa na Wajerumani, maandishi yalibadilishwa mara kadhaa. Maonesho ya katalogi yanaelezea mmiliki wa kiti kama ni mke wa mtawala. Hivyo, nafasi halisi ya mamlaka ya mmiliki wa zamani iliendelea kufanywa isionekane. Lakini hali halisi ya mwanamke ambaye nyumba yake pamoja na vitu vingine vilivyoporwa alikuwa na hali gani? Je, tunaweza kupata hitimisho kutoka kwa mmiliki wa kiti kuhusu hali yake ya kijamii? Je, kitu hicho kinaweza kuwa kiti cha mtawala wa kike?

— Kiti cha mwanamke mashuhuri · Tanzania, Urugu (Wembere) · karne ya 19. · mbao · sm 107 × 43 × 44 · watengenezaji, watumiaji, walinzi, wamiliki: msanii asiyejulikana; mwanamke mashuhuri kutoka Urugu mpaka (?); Gideon von Grawert mpaka 1898; uliofanyika tangu 1898 na Jumba la Makumbusho la Königliches Museum für Völkerkunde, Berlin (Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, III E 6720)



Picha 41

'KITU' HIKI HUENDA NI KITI CHA KIONGOZI WA KIKE?

JE, NI KITI CHA ENZI? URUGU IPO WAPI LEO?




Picha 42

Je, ni kwa jinsi gani pambo la kuvutia la sikio la mbao la *Mangi* Marealle pamoja na sanduku lake lililopambwa na shaba lilikuja kumilikiwa na mchapishaji tajiri wa Leipzig Hans Meyer?
Vyanzo vilivyochunguzwa hadi sasa havijatoa maelezo. Je, kitu hicho kilikuwa na umuhimu gani na kazi gani kwa *Mangi* Marealle, aliyetawala Marangu tangu mwaka 1880 na kuendelea, na ilihusishwa vipi na hadhi yake kama *mangi*?

Bila kujua majibu ya maswali haya hatuwezi kusema kwa uhakika kama kitu hicho kilichochukuliwa kinaweza kuuzwa. Yamkini Marealle alimpa pambo la sikio Meyer kwasababu alidhani ni muhimu kuanzisha mahusiano mazuri na washirika wa kikoloni wa Kijerumani. Waheshimiwa kama Marealle walitaka kudai masilahi yao katika mazingira yenye malipo ya juu ya ushirikiano na upinzani. Hivyo, pambo la sikio lilikuwa pia ni kitu kimojawapo cha mchakato wa mazungumzo ya kikoloni na mahusiano (mamlaka).



— Katalogi kuu ya kihistoria ya Makumbusho ya Ethnolojia Berlin (Ethnologisches Museum Berlin) imemuorodhesha Hans Meyer kama "mfadhili", huku Mangi Marealle akionekana katika maelezo hayo kama mvaaji wa pambo hilo la sikio. Majina hayatajwi sana kuhusiana na vitu zaidi ya 8000 kutoka Tanzania bara ambavyo vilimilikiwa wakati wa ukoloni wa Wajerumani na Waingereza. Waundaji wengi, wamiliki na watumiaji wa vitu hubakia bila majina. Kwa ujumla "wakusanyaji" wa Ujerumani na Ulaya walitaja waheshimiwa kutoka Afrika Mashariki na kutaja mahusiano yao na vitu. Wanawake katika nyadhifa za kisiasa ni nadra sana kuonekana katika kumbukumbu za kikoloni. Wengi wao hubaki bila majina au hupuuzwa moja kwa moja. Baadhi ya vitu hivi vilikuwa vinabaki na kumbukumbu ya tuzo.

— Kuanzia miaka ya 1890, Mangi Marealle alitumia wawakilishi wa dola ya kikoloni ili kuwezesha mifumo itakayofanya kazi ili kumwezesha kushika hatamu za mamlaka ya kisiasa. Aliamua kuimarisha upinzani wake kwa Wajerumani na hivyo akajiimarisha kwenye nafasi yake kihairakia katika serikali ya kikoloni na hatimaye akawa ndiye Mangi pekee mwenye nguvu huko Kilimanjaro Mashariki mwaka 1890. Alitawala koo 27 kati ya koo 44 za Wachaga walioishi karibu ya Kilimanjaro na akapata jina la utani Kilamia, "mshindi". Lakini hadhi ya Marealle haikuwa thabiti kwani alikuwa akitegemea fadhila za Chifu aliyewekwa na Wajerumani huko Moshi. Kampeni za kijeshi dhidi ya Mangi zikapangwa kutokana na kutoonesha ushirikiano kwa Wajerumani jambo ambalo lilikuwa la muhimu sana katika utawala wa kikoloni. Marealle aliachwa kwenye cheo kikubwa mwaka 1912.

## JE, MAREALLE ALIKUWA NA UHUSIANO GANI NA PAMBO HILI LA SIKIO?



Picha 43



Picha 44



— Pambo la sikio · Tanzania, Marangu (Kilimanjaro) · karne ya 19. · mbao, shaba · sm 1.2 × 8.2 × 8.4 · watengenezaji, watumiaji, walinzi, wamiliki: msanii asiyejulikana; *Mangi* Marealle wa Marangu hadi mwaka 1887 au 1889; Hans Meyer kuanzia mwaka 1897; umiliki ulishikiliwa tangu mwaka 1897 na Jumba la Makumbusho la Königliches Museum für Völkerkunde, Berlin (Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, III E4815)

JE, ALIKUWA NA HAKI YA KULITOA NA KUMKABIDHI MTU ASIYEMJUA?

NIA YAKE ILIKUWA NI NINI KUMPATIA KITU HICHO HANS MEYER?

# MINGLED LIVING FORCES

## VIKOSI HAI VILIVYOCHANGANYIKA. UINGILIAJI MPYA WA KISANAA KAMA SEHEMU YA WARSHA YA MAONESHO “KUONYESHA.KUTOKUWEPO” (MACHI 11–JULAI, 2023)

Ni kwa namna gani tunaweza kusawiri kisanaa masalia ya vurugu za kikoloni? Je, ni kwa vipi msanii anaweza kuingilia kati makumbusho ya kiethnolojia yakarejesha mali za kitamaduni zilizoibwa pamoja na mabaki ya binadamu? Je, tunawezaje kukisia yatakayotokea kwa siku zijazo?

Kuna zaidi ya ‘vitu’ 10,000 kwenye Makumbusho ya Ethnolojia Berlin ambavyo vinahusishwa na Tanzania ya sasa. Idadi kubwa ya hivi ‘vitu’ viliporwa wakati wa enzi ya utawala wa kikoloni wa Mjerumani na Mwingereza. Warsha ya maonesho ya *“Kuonyesha.Kutokuwepo – Vitu kutoka Tanzania na Nyaraka za Kikoloni”* imetupatia mkabala mpya wa kuuliza maswali, kukumbuka, na kutafakari kuhusu ‘vitu’ viliyofanywa na makumbusho pamoja na kusimulia hadithi zake. Kama sehemu ya maonesho, wanafunzi walitathmini vuruga za wakoloni kupitia kuingilia kati yaani “Vikosi hai vilivyochanganyika”. Walitumia sanaa za maonesho, mitambo, uchapishaji, uchongaji, uchoraji, video, na ukweli wa kuona ili kuchunguza umuhimu wa kukusanya na kuonesha katika muktadha wa utawala na kuendeleza mahusiano ya kikoloni. Hata hivyo, waliakisi namna makumbusho inavyoweza kufanya kazi kwa baadaye hasa mabaki ya binadamu pamoja vitu halisi vya kitamaduni vitakaporudishwa.




“Vikosi hai vilivyochanganyika” iliundwa kama sehemu sanjari ya semina kuhusu “Uwepo wa Ukoloni: Mazungumzo Kisanaa na Kihifadhi” na “Zeichnen Farbe Fläche – Spatial Drawing” kwenye weißensee kunsthochschule berlin wakati wa semesta ya majira ya baridi mwaka 2022/23. Juana Awad, kutoka Idara ya Nadharia na Historia, na Elaine Bonavia, kutoka Idara ya Ubunifu wa Mavazi – na Usanifu wa Majengo, walihusika na kuwajibika kwa mchakato wa utunzaji na ufundishaji.




Picha 45






Picha 46

# KUONYESHA.KUTOKUWEPO. KUFIKIRIA ZAIDI

## KUINGILIA KATI KULIKOFANYWA NA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA HUMBOLDT CHA BERLIN (KUANZIA TAREHE 19.10.2023)

Ni kwa vipi maonesho ya muktadha wa ukoloni yanaweza kusanifiwa? Je, ni vitu gani vinafaa kuoneshwa kabisa na kwa vipi tunaweza kushughulikia utupu na vurugu za kikoloni ambavyo vimeonekana kwenye vitu vingi?

Wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Humboldt cha Berlin walichunguza maswali haya katika semina ya 'Kuchunguza Ukoloni' katika semesta ya majira ya baridi 2022/23. Majadiliano ya kina yaliyotokana na mhadhara yalifuatiwa na utambuzi wa vitendo na muundo wa majadiliano. Katika muktadha huu, wanafunzi walifanya mahojiano na wataalamu waliochaguliwa, na pia waliandaa paneli za mijadala ya umma na kuchambua kiyakinifu dhana za maonesho zinazotumiwa na makumbusho ya Berlin. Mfano mzuri ni Museum Treptow au FHXB Friedrichshain-Kreuzberg Museum vyote viko Berlin.
Pia sehemu muhimu ya semina hii ilikuwa ushirikiano na timu ya usimamizi wa "Kuonyesha. Kutokuwepo". Hii ilioneshwa kuanzia Oktoba 2022 hadi Machi 2023 kupitia kutembelea tovuti nyingi, kufanya majadiliano, vikao na semina na kazi ya kikundi katika sehemu za maonesho. Michango ya wanafunzi inayotokana na kazi hii imekuwa na nafasi ya kudumu katika maonesho haya tangu Oktoba 2023. Hizi ni pamoja na hatua, kama vile maonesho na maswali kuhusu kuthibitika kwa 'miradi' (Mchoro 48), maoni juu ya 'vitu' vya mtu binafsi na 'miradi', kama vile bango kwa ajili ya komode ya mihuri (Mchoro 49), au nyongeza na upanuzi wa vipengele vya maonesho vilivyopo, kama vile kituo cha kupigia picha (Mchoro 47). Tukio hilo liliandaliwa na Janis Nalbadidacis kutoka Taasisi ya Sayansi ya Kihistoria katika Chuo Kikuu cha Humboldt cha Berlin.

Ufahamu zaidi juu ya mawazo na maoni ya wanafunzi na kozi inaweza kupatikana katika kiungo kifuatacho: https://moodle.hu-berlin.de/course/view.php?id=117728



Picha 47



Picha 48






Picha 49

## ORODHA MUHIMU YA MAANDISHI

Lugha ina nafasi kubwa katika maonesho. Tumeweka baadhi ya miongozo kwa ajili ya kutusaidia kuandika matini kwa ajili ya maonesho:

– MAJINA YANAYOZINGATIA JINSIA au "kupunguza jinsia":
Endapo haitakuwa rahisi kuweka wazi kwamba kikundi kinachozungumziwa kinawahusu wanaume pekee, lugha jumuishi inayozingatia jinsia itatumika au lugha isiyopendelea jinsia itatumika.

– MAJINA YA HESHIMA kwa ajili ya mambo yote yanayohusu tamaduni na dini na mitazamo yatazingatiwa bila kutumia lugha ya hukumu.

– NAFASI:
Ni nani anaongea? Ni nani anaandika na anaandika kwa kutumia mtazamo gani? Je, mwandishi anajizuia kutumia mtindo wa uandishi unaodai kutoegemea upande wowote? Maneno muhimu: Mtazamo wa Kiulaya, mahusiano ya kawaida (mwanamume na mwanamke), na ulemavu umeinuliwa hadi kiwango cha kawaida (hakuna ubaguzi wa ulemavu). Je, hizo lebo zinarejelea waandishi ambao ni weupe?

- MATUMIZI YA KAULI ZA UTENDWA na KUJIZUIA KUTUMIA "nafsi ya kwanza":
Kwa kutumia kauli ya utendwa, mwandishi anaweza kukwepa kuwataja watendaji weupe (kwa mfano. "Bolivia inanyonywa.") na kwa namna hiyo inadhihirisha mtazamo wa Kiulaya au kupingana na mitazamo ya wengine (kwa mfano, "Marekani iligunduliwa mwaka 1492.").

– KUACHILIA MAMLAKA YA UKALIMANI:
Kwa kadri inavyowezekana, je watu wana uwezo wa kusema kwa kutumia nukuu au mahojiano au kwa kuandika maandishi yao wenyewe?

– KUZUIA UJUMUISHWAJI:
Je, kuna uwezekano wa kutoa maelezo mahususi ya hali iliyopo, badala ya kufanya ulinganifu na ujumuishwaji (kwa mfano, "Umaskini umeenea Afrika.")

– Je matini zimetungwa kwa KUSHIRIKIANA au kwa mtindo wa maamuzi ya mtu mmoja?

– Je, watu WANAWASILISHWA AU KUELEZEWA kwa usahihi kama watendaji (wahusika) katika UTATA wao badala ya kudunishwa kupitia vitu vinavyowaathiri kama vile umaskini, "makabila", au ulemavu? Je, maandishi yanajizuia kusema vitu vinavyomfanya mtu ajisikie vibaya *(klinchezi)*?

–Je kuna maana yoyote kati ya UHUSIANO unaojengwa sasa na UKOLONI ULIOPITA? Muundo wa kikoloni nje ya muktadha wa mfumo wa kikoloni wa Mjerumani unatakiwa uonekane waziwazi.

– Je istilahi zote muhimu zimechaguliwa kwa umakini? Je, maandishi yanaakisi ukweli kwamba LUGHA INAPENDELEA? Kwa kubadilisha mtazamo inaweza kusaidia uchaguzi wa istilahi! Je, ninaweza kutumia istilahi mahususi ya kikabila ili kuelezea hali yangu?

– Jizuie kurudia taasubi na mila potofu zilizopo zinazodhaniwa kuwa ni kinyume: kupinga watu wa Ulaya, kupinga watu wengine, uhusiano wa mazingira-watu, n.k.

– Tumia istilahi zilezile, lebo, na maelezo ambayo ungeyatumia kuwaelezea watu wa Ulaya na hali zao.

– Kuacha nguvu ya ufafanuzi: Tumia istilahi ambazo vikundi au jamii watapenda kuzitumia kujizungumzia wao wenyewe.

– Jizuie kutumia istilahi za ubaguzi wa rangi na wa ulemavu: Unapopatwa na mashaka, tumia faharasa ya ufafanuzi na uliza wataalamu kwa ajili ya maoni yao kuhusu jambo husika.

TAFADHALI ZINGATIA:
Mawazo ya kibaguzi kwa misingi ya rangi yanaweza kuwakilishwa na istilahi fulanifulani ("kabila", au "utamaduni" badala ya "rangi").

“Hatutaki kuangalia vitu vilivyoporwa na kufurahia maisha ya upendeleo. Tunataka ufafanuzi utolewe na watu! Kuwa kisemeo! Kataa unyonyaji!” (mgeni)

“Tafadhali rudisheni sanaa zilizoibwa!” (mgeni)

„Kwa nini urejeshaji ni mgumu?“ (mgeni)



„Ninataka kuwajulisha ni kwa kiasi gani nimefurahishwa na namna mnavyotambua & kujitofautisha na muktadha wa kikoloni ambao mradi wenu mnaouonesha. [...] Ningetamani kama kungekuwa na sehemu kubwa zaidi katika kila chumba ili kuweka nakala ya hizi sanaa pamoja na sanaa zenyewe ambazo ni halisi.” (mgeni)

“Kwa nini serikali ya Ujerumani haivirudishi vitu vilivyoibwa?” (mgeni)

“Nilidhani hapa ni pazuri sana (mgeni)

"Je, ni kitu gani kimeshafanyika ili kurekebisha udhalimu wa wakoloni?"
(mgeni)

"Linapokuja suala la kurudisha vitu, ni kwa nini nchi zilizotawaliwa kwa kutumia vurugu/watu wake wanatakiwa wathibitishe hivyo vitu ni vya kwao na siyo vya Humboldt Forum?"
(mgeni)



"Toeni nakala ya sanaa zilizoibwa kisha warudishieni vitu vyao halisi!"
(mgeni)

"Lazima kuwe na maonesho ya vitu vilivyorejeshwa Tanzania."
(mgeni)

# HITIMISHO

kwa Vicensia Shule (Mshauri Mkosoaji)

Mchakato wa kuratibu “Kuonyesha.Kutokuwepo” na kuwasilisha kwa umma ilikuwa ni safari yenye changamoto nyingi na mafunzo tele. Methodolojia iliyotumika katika kila hatua ambayo timu ya wahifadhi ilipitia, na ilikuwa ni fursa pekee ya kupokea mirejesho na maoni yaliyopendekezwa.

Mchakato wa kuratibu warsha hii ya maonesho siyo wa kawaida na hivyo inahitaji utafiti zaidi na kufuatilia kwingi. Pia maonesho kama tokeo la mwisho ni kitu kipya kwa wageni wanaotembelea makumbusho ambao walizoea kuona vitu halisi/rasilimali. Kuna haja ya kutangaza methodolojia zilizotumika kwenye maonesho. Kuna haja ya kutafiti zaidi kuhusu athari ya mkabala wa “Hakuna Idhini – Hakuna Kitu” kwa pande zote mbili; kwa wamiliki wa hizo mali wa huko Tanganyika, ambayo kwa sasa ni Tanzania na pia Ujerumani.

Hata ile dhana pana ya ‘kuonyesha’ vitu vya watu na mali zao, ambavyo vilichukuliwa kwa vurugu, kuiba na kudanganya, inahitaji utafiti wa kina zaidi. Je, tunaweza kundelea kujisifia kwa vitu vya wizi na kuwatukuza wahalifu waliovileta vitu hivi kwa jina la wakusanyaji? Kabla hatujafikiria kuonesha vitu hivi, ni lazima tujaribu kuvaa viatu vya wale watu ambao walipoteza ndugu zao kutokana na Wajerumani kulipiza kisasi kwa wapigania uhuru wa Tanganyika kama ilivyotendeka katika Vita vya Maji Maji dhidi ya Wajerumani walipovamia Tanganyika kuanzia mwaka 1905–1907.



Kama ambavyo tunaendelea kuponya majeraha kupitia simulizi hizi za ukoloni wa Mjerumani huko Tanganyika, itakuwa ni busara tuzipitie upya istilahi za kawaida ambazo zinajulikana kama ‘vitu’ ili kurejelea mali zilizoibwa na kuchukuliwa wakati wa ukoloni na baada ya hapo. Mali nyingi zilizochukuliwa kutoka Tanganyika wakati wa uvamizi wa kikatili wa Wajerumani havioneshi wamiliki ni akina nani; bali tuna majina ya watu waliozipeleka mali hizo Ujerumani, “mkusanyaji”. Tunaporejea dhana ya ridhaa, je ni ridhaa ya nani inayomaanishwa na kurejelewa hapo?

Hili suala la kuondoa simulizi za kikoloni za Wajerumani linatakiwa kuchukuliwa kwa uzito zaidi kwa kurudisha kwa fidia kubwa uharibifu uliotendeka. Ni lazima tuzungumzie suala la mahusiano ya kimamlaka, kwa waliotawaliwa na waliowatawala kwa uzito sawa sawia.



Picha 50

# HISTORIA YA MRADI

Miradi ya kushirikiano na utafiti ya Ethnologisches Museum, Staatliche Museen zu Berlin – Stiftung Preußischer Kulturbesitz pamoja na taasisi mbalimbali na watendaji nchini Tanzania:

2016–2018: HUMBOLDT LAB TANZANIA (MAABARA YA HUMBOLDT TANZANIA)
Kwa kushirikiana na washirika: University of Dar es Salaam; Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam na Makumbusho ya Kumbukizi ya Vita vya Maji Maji, Songea; Nafasi Art Space; Bookstop Sanaa Visual Art Library & Creative Learning Space, Dar es Salaam; Goethe-Institut Tanzania; vizazi vya waandishi, watumiaji, walezi na wamiliki wa 'vitu'

2016–2021: TANZANIA / UJERUMANI: Kushirikishana Hadithi za 'vitu'? Kwa kushirikiana na washirika: University of Dar es Salaam; Makumbusho ya Taifa la Tanzania; Nafasi Art Space, Dar es Salaam; Bookstop Sanaa Visual Art Library & Creative Learning Space, Dar es Salaam



2019–2022: UTAFITI KWA KUSHIRIKIANA WA 'VITU' VILIVYOKUSANYWA
kutoka Tanzania katika Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni Dar es Salaam na Ethnologisches Museum, Staatliche Museen zu Berlin Kwa kushirikiana na washirika: University of Dar es Salaam; Makumbusho ya Taifa la Tanzania; vizazi vya waandishi, watumiaji, walezi na wamiliki wa 'vitu'.

2019–2023: MALI INAYOGOMBANIWA: Mguso na Hisia katika Migogoro ya Kikanuni ya Tamaduni Tofauti kuhusu Makusanyo ya Kiethnografia katika Jukwaa la Humboldt (SFB 1171 Affective Societies)
Kwa kushirikiana na washirika: Freie Universität Berlin, Charité – Universitätsmedizin Berlin; Martin-Luther-Universität Halle-Wittenberg; Max-Planck-Institut für Ethnologische Forschung; Botanischer Garten & Botanisches Museum Berlin; Universität Hamburg; vizazi vya waandishi, watumiaji, walezi na wamiliki wa 'vitu'.

KUTOKA 2022: WAZO NA UTAFITI KWA AJILI YA MAONESHO YA PAMOJA "HISTORIA YA TANZANIA" (JINA LA KUFANYIA KAZI)
Kwa kushirikiana na washirika: Maafisa waangalizi kutoka Makumbusho ya Taifa la Tanzania, na Ethnologisches Museum – Staatliche Museen zu Berlin na Stiftung Humboldt Forum; wataalamu na vizazi vya waandishi, watumiaji, walezi na wamiliki wa 'vitu' nchini Tanzania

# ORODHA YA VIELELEZO

Haki za picha za chapisho hili zimefanyiwa utafiti na kupatikana kwa ujuzi wetu wa hali ya juu. Ikiwa, licha ya juhudi zetu hizi bora, wamiliki wa hakimiliki hawajapatikana, tafadhali toa habari husika ili waweze kuwasiliana na data iliyosasishwa. Tungependa kuwashukuru watu wote binafsi, nyaraka zote, taasisi zote ambao wamefanya picha hizo zipatikane kwetu.

Jalada: Indeksi Kuu ya Historia, "Liste der Objekte einer ostafrikanischen Würdenträgerin aus Urugu" (Orodha ya vitu alivyomiliki Mwanamke mashuhuri wa Afrika Mashariki kutoka Urugu), © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum (HK Afr 23) / CC BY-NC-SA 4.0; picha imepigwa upya na Szandra Tebbe / Studio Ra / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss

Ukurasa ya 2 na 3: Ramani ya Dunia, 2022, © Kartographie Peckmann; picha imepigwa upya na Martiene Raven / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss

Picha 1: Rekodi za mkutano wa Zoom pamoja na Jocelyne Stahl, Maike Schimanowski, Kristin Weber-Sinn, Paola Ivanov, Josephine Apraku na Vicensia Shule (kutokea juu kulia kuelekea chini kushoto) tarehe 24 Septemba 2021, huko Berlin na Arusha.

Picha 2: Mwonekano wa kabati za Maonesho, picha, 2023, Berlin, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Pich 3–4: rasimu ya dhana ya kubuni, mfano, 2024, Berlin, © Szandra Tebbe / Studio Ra

Picha 5: Haijulikani, Sahani ya shaba yenye maandishi ya mji wa Kilwa Kisiwani, katika Georg Braun, Frans Hogenberg, Civitates orbis terrarum (atlasi yenye miji ya dunia), Cologne 1593, © Universitätsbibliothek Heidelberg, public domain

Picha 6: Haijulikani, Ramani ya Tanganyika ikionesha makundi mbalimbali ya umma katika muktadha wa kikoloni, katika John Iliffe, *A Modern History of Tanganyika*, Cambridge 1979, p. xvi, © Cambridge University Press

Picha 7: "Indischer Händler vor seinem Geschäft" (Mfanyabiashara wa Kihindi mbele ya duka lake), slaidi (diyapositivu), b/w, mm 60 × 90, 1908, mpigapicha: Robert Lohmeyer © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum (VIII A 1617), CC BY-NC-SA 4.0

Picha 8: "Der mächtige ostafrikanische Händler Machemba bin Mshame al Masaninga" (Mfanyabiashara mashuhuri wa Afrika Mashariki Machemba bin Mshame al Masaninga), Dar es Salaam (?), positive ya kusafishia picha, b/w kwenye kadibodi, 1896, imechapishwa na C. Vincenti, Dar es Salaam, from the estate of Ch. Porrée, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum (VIII A 21940), CC BY-NC-SA 4.0

Picha 9: Mwonekano wa kabati za Maonesho, picha, 2024, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 10: Vitu vilivyo na eneo katika Makumbusho ya Ethnolojia Berlin na kumbukumbu ya kijiografia ya Tanzania kwa mwaka wa ununuzi, 2017, © Hendryk Ortlieb, Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum

Picha 11–16: Picha za filamu kutokana na dokyumentari ya nyenzo za uhifadhi, 2022, Berlin, © Josephine Apraku / David Buchholz / tellsomemore production, 2022

Picha 17: "Dampfpflug" (Jembe la mvuke), Tanzania, Saadani, picha ya karatasi, b/w, sm 13 × 18, mwaka 1907, mpigapicha: hajulikani, ilikusanywa na Bernhard Dernburg, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum (VIII A 18356), CC BY-NC-SA 4.0

Picha 18: Mwonekano wa maonyesho, picha, 2023, Berlin, © Julija Goyd

Picha 19: "Baumwollernte" (Mavuno ya Pamba), Tanzania, Saadani, picha ya karatasi, b/w, sm 13 × 18, mwaka 1907, mpigapicha: hajulikani, ilikusanywa na Bernhard Dernburg, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum (VIII 18438), CC BY-NC-SA 4.0

Picha 20–23: Mwonekano wa zinesi kwenye maonesho, picha, 2024, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Aditya Sah

Picha 24: Mwonekano wa kituo cha redio ya kianalogia kwenye maonesho, picha, 2024, Berlin, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 25: "Unter den Akazien" (Chini ya mti wa mshita), Dar es Salaam, Tanzania, picha ya karatasi, b/w, 1896, mpigapicha: hajulikani, ilichapishwa na C. Vincenti, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum (VIII A 21929), CC BY-NC-SA 4.0

Picha 26: Maonesho ya Idara ya Afrika (Cameroon), Museum für Völkerkunde Berlin, picha ya karatsai, b/w, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum

Picha 27: Kaznidata kwa III E 6718, "Zapfentür" (mlango) unamilikiwa na mwanamke mashughuli, picha ya skrini, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum

Picha 28: Karatasi yenye taarifa za kweli kutoka kwenye kanzidata ya makumbusho ikionyesha taarifa ya kiko kilichomilikiwa na *mtemi* Mirambo, tarehe 6 Mei, mwaka 2022, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, picha imepigwa upya na Szandra Tebbe / Studio Ra / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss

Picha 29: mchoro wa thread, kielelezo, Berlin, 2022, © Szandra Tebbe / Studio Ra / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss

Picha 30, 32, 33: Mwonekano wa maonyesho, picha, 2022, © Julija Goyd

Picha 31, 34: Mwonekano wa maonyesho, picha, 2024, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König



Picha 35: Takwimu ya binadamu, mbao, kabla ya urefu wa 1869 x upana x kina: 114 x 31 x 16,5 cm, uzito: 21,5 kg, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, (III E 5529) / Heini Schneebelo, CC BY-NC-Sa 4.0

Picha 36: Mwonekano wa kibadala cha *kigiilya* 'kitu' kwenye maonyesho, picha ya 3D, bloko ya poluliretheni bloko, kwa vipimo sahihi, 2022, © Werk 5 GmbH / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 37: Mfuko na ‚vitu' vya dawa, ngozi ya wanyama, raffia, undated (kabla ya 1907), urefu x upana x kina: 40 x 20 x 26 cm, uzito: 2,4 kg (jumla ya uzito), © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, picha: Martin Franken

Picha 38: Mtazamo wa mfuko na ‚vitu' vya dawa kama ‚kitu' cha surrogate katika maonyesho, imesanifiwa na Amani Abeid, dondoo kutoka riwaya ya picha Nkoba, vyombo mbalimbali vya habari, Dar es Salaam, Tanzania, 2022, © Amani Abeid / Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 39: Gamba la riwaya picha *Nkoba*, Dar es Salaam, Tanzania, 2022, © Amani Abeid, Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum

Picha 40: Mwenyekiti wa sultaness wa Urugu, mbao, karne ya 19, urefu x upana x kina: 107 x 43 x 44 cm, uzito: 8,2 kg, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum, picha. Martin Franken

Picha 41: Picha ya mwenyekiti wa sultaness wa Urugu kama ‚kitu' cha surrogate katika maonyesho, iliyoundwa na Szandra Tebbe / Studio Ra, njama ya foil, kweli kwa kiwango, 2022, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 42: Kito cha sikio, mbao, shaba, undated, urefu x upana x kina: 1,2 x 8,2 x 8,4 cm, ukubwa wa 'kitu': cm H: 1 cm, D: 8,2 cm, uzito: 21 g, © Staatliche Museen zu Berlin, Ethnologisches Museum / Anna-Isabel Frank, CC BY-NC-SA 4.0

Picha 43: Picha ya Marealle, picha, Marangu, 1887, mpigapicha: Hans Meyer, © Sächsische Landesbibliothek – Staats- und Universitätsbibliothek Dresden, Deutsche Fotothek, Hans Meyer

Picha 44: Mwonekano wa kito cha sikio kama kibadala cha 'kitu' kwenye maonyesho, picha ya 3D, bloko ya poluliretheni bloko, kwa vipimo sahihi 2022, © Werk 5 GmbH / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 45: Mwonekano wa kuingilia kati kwa "Vikosi hai vilivyochanganyika", picha, 2023, © imad Amalfi, Bar Esh, Quang Vinh Giang, Jasmin Sermonet, Inyeong Song, Jelisa Weber / Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 46: Bango la kuingilia kati la "Vikosi hai vilivyochanganyika", 2023, © weißensee kunsthochschule Berlin

Picha 47-49: Mwonekano wa maonesho yakionyeshwa kazi za wanafunzi wa Humboldt-Universität, picha, 2024, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, picha: Andreas König

Picha 50: Mshauri Mkosoaji Vicensia Shule (katikati) katika mazungumzo na wasimamizi Jocelyne Stahl (kushoto) na Maike Schimanowski (kulia), picha, 2022, © Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, Maike Schimanoski

# CHAPA

Kuonyesha.Kutokuwepo – Vitu kutoka Tanzania na Nyaraka za Kikoloni

Maonesho ya muda ya Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss kwa ushirikiano na jumba la makumbusho la Ethnologisches Museum kwenye Staatliche Museen zu Berlin – Preussischer Kulturbesitz

Imefadhiliwa na Federal Government Commissioner for Culture kwa kuzingatia azimio la Bunge la German Federal Parliament.

Mchapishaji: Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss

Waandishi: Josephine Apraku, Paola Ivanov, Ulrike Kirsch, Maike Schimanowski, Vicensia Shule, Jocelyne Stahl, Kristin Weber-Sinn

Mhariri na Msimamizi wa mradi: Franziska Lukas

Kopiedita: Silke Körber

Wafasiri: Silke Körber, Elizabeth Mahenge, Tradukas GbR

Mhariri wa picha: Barbara Martinkat

Msanifu: Szandra Tebbe (Studio Ra)

© Berlin 2026 Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss, Schlossplatz, 10178 Berlin, www.humboldtforum.org

Maonesho ya timu ya wahifadhi: Paola Ivanov, Ulrike Kirsch, Maike Schimanowski, Jocelyne Stahl, Kristin Weber-Sinn

Washauri wa kukosoa: Josephine Apraku, Vicensia Shule

Maonesho ya timu ya mradi: Nadine Ney, Franziska Lukas, Maria Mazgaj, Noelle von Galen, Anne Jänichen, Luise von Bresinski, Johanna Kapp, Maike Voelkel, Eva Ritz

Programu ya timu ya maafisa waangalizi: Annelie Mattheis, Maike Schimanowski, Jocelyne Stahl, Uta Kornmeier

Programu ya uzalishaji: Grusche Gregor, Rebekka Straub

Muundo wa maonesho, mazungumzo ya dhana ya usimamizi, michoro ya maonyesho, vielelezo na mwangaza: Szandra Tebbe & Team (Studio Ra)
Timu ya mandhari: Gregor Müller, Guido Spriewald,
Picha za timu ya maonyesho, picha zenye maelezo: Tim Grützner, Katharina Triebe, Elie Peuvrel, Martiene Raven, Vyombo vya habari: Abdalla Khamis Abdalla, Josephine Apraku, David Buchholz (tellsomemore production), EIDOTECH GmbH, Simone Nowicki, Daniela Prochaska, Albrecht Wiedemann

Utunzaji wa sanaa: Ute Freitag (Büro für kleinteilige Lösungen)

Ushauri jumuishi: Nina Kadri, Friedrun Portele-Anyangbe, Ulrike Rau (raumkonzepte)

Uhariri na usahihishaji matini za maonesho: Dagmar Deuring, Tanja Milewsky

Maonesho ya matini zilizotafsiriwa: Tradukas GmbH, Elizabeth Mahenge & Team (swahilispeaking.co.tz)

Taasisi ya mikopo: Staatliche Museen zu Berlin / Stiftung Preußischer Kulturbesitz Berlin

Tunapenda kuwashukuru wafuatao kwa ushauri na usaidizi wao wa kitaalamu: Abdalla Khamis Abdalla, Amani Abeid, Josephine Apraku, David Buchholz, Jim Chuchu, Colonial Presents Seminar der weißensee kunsthochschule berlin, Michael Dieminger, Vincent Engel, Leah Fischer-Swierczynski, Hanin Hannouch, Victor Kégli (50Lux), Arseniy Khudyakov, Elizabeth Mahenge, Nicholas Calvin Mwakatobe, Simone Nowicki, Amel Ouaissa, Kartographie Peckmann, Daniela Prochaska, Rost: Werbetechnik GmbH, Florian Saul, Seminar „Kolonialismus ausstellen" des Instituts für Geschichtswissenschaften, Humboldt Universität zu Berlin, Elisabeth Seyerl, Vicensia Shule, Walkenbach und Heyer GmbH, Albrecht Wiedemann

Kwa umahususi kabisa, tungependa kuwashukuru wapatanishi wa kujitegemea wanaofanya kazi katika maonesho. Tunapenda kuwashukuru wafanyakazi wa Stiftung Humboldt Forum im Berliner Schloss na wa Jumba la Makumbusho la Ethnologisches Museum kwenye Staatliche Museen zu Berlin pamoja na wale wote ambao hawajatajwa hapa kwa majina ambao wamechangia katika mafanikio ya mradi huu.

ISBN 978-3-9828472-2-1
DOI https://doi.org/10.61060/9783982847221-SHF-03

STIFTUNG HUMBOLDT FORUM IM BERLINER SCHLOSS

Staatliche Museen zu Berlin
Preußischer Kulturbesitz

Gefördert durch:

Die Beauftragte der Bundesregierung für Kultur und Medien

aufgrund eines Beschlusses des Deutschen Bundestages

‘Vitu’ vingi kutoka Tanzania ambavyo viko katika makumbusho huko Ujerumani Ethnologisches Museum Berlin viliibwa, viliporwa, vilinyang’anywa, vilinununuliwa, au vilitolewa kama zawadi na/au vilifanyiwa biashara katika muktadha wa mahusiano yasiyo na usawa chini ya utawala wa kikoloni wa ama Wajerumani au Waingereza. Tunadhani kwamba hakuna ridhaa iliyotolewa kwa vitu hivyo kuonesh-wa kwenye maonyesho.

Nani anapaswa kutoa ridhaa ya kuonesha kwenye maonesho yao?
Je ni wapi vilichukuliwa na je ni mali ya nani ‘vitu’ ambavyo vinashikiliwa kwenye bohari ya makumbusho?
Je, vilipatikana na vilimilikiwa kwa njia gani?
Je, wakoloni walipuuza historia gani?
Nani alinufaika na mfumo dhalimu wa kikoloni?
Ni kwa namna gani muundo na fikra za kibaguzi unaendelea kuathiri jamii hivi leo?
Je, ni nani ana maamuzi kuhusu uwakilishi wa makundi na jamii?
Ni kwa namna gani kukosekana kwa ridhaa ya hivi ‘vitu’ kunavyoathiri uonyeshwaji kwenye makumbusho?
Ni kwa namna gani makumbusho ni ya kikoloni?

Timu ya wahifadhi pamoja na *washauri wakosoaji*, waliachambua na kujadili maswali haya na mengine kama sehemu ya warsha ya maone-sho ya „Kuonyesha.Kutokuwepo– Vitu kutoka Tanzania na Nyaraka za Kikoloni“. Maonesho yalifanyika kuanzia Septemba mwaka 2022 hadi Juni mwaka 2024 huko Ujerumani Berlin’s Humboldt Forum.